# Nipashe

Jumatatu Mei 2, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580933
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US










## Aliyetuhumiwa kuua mke akutwa amejinyonga porini

UKURASA 8



Rais Samia Suluhu Hassan akiwahutubia wafanyakazi katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani yaliyofanyika kitaifa jijini Dodoma jana. **PICHA: WIZARA YA FEDHA**

### NYONGEZA MISHAHARA

# Samia: Jambo letu sasa lipo

• **TUCTA** yawasilisha kwake kilio cha kikokotoo... *Endelea ukurasa 2*




Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka akiongoza maandamano katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani jana. **PICHA: ADAM MZEE**



Katibu Mtendaji NECTA, Dk. Charles Msonde

# NECTA kuanza kusahihisha mitihani kidijitali mwezi huu

UKURASA 4

**MICHEZO** **INONGA: SIKUTAKA MAYELE 'ATETEME'** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan, akisalimiana na vikosi mbalimbali vya ulinzi katika sherehe za Mei Mosi, jana Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Rais Samia: Jambo letu lipo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu amesema suala la upandaji wa mishahara kwa wafanyakazi mwaka huu lipo, lakini halitakuwa kwa kiwango ambacho kimependekezwa na Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi (TUCTA).

TUCTA iliomba kiwango cha chini kiwe Sh. 1,010,000 kwa mwezi kwa mfanyakazi kutokana na kupanda kwa gharama za maisha.

Akizungumza jana katika sherehe za wafanyakazi nchini, Rais Samia alisema: "Lile jambo letu lipo, ila si kwa kiwango kilichosemwa na TUCTA kwa sababu mnajua hali ya uchumi wa nchi yetu, hali si nzuri sana uchumi wetu ulishuka chini mno, tumejitahidi sana kwa sababu nilishatoa ahadi mwaka jana nimeagiza jambo hili liwepo."

Alisema "Mahesabu yanaendelea tutajua lipo kwa kiasi gani, lakini jambo lipo."

Rais Samia alisema ujumbe wa maslahi ya wafanyakazi umekuwa ukiwasilishwa kwenye maadhimisho ya aina hiyo miaka kadhaa, lakini kwa mwaka huu wameyatumia kama kauli mbiu.

"Kuhusu viwango vya mshahara ninakubaliana nanyi kabisa kwamba vya sasa havikidhi mahitaji ya mfanyakazi pamoja na familia yake husan nyakati kama hizi ambazo gharama za maisha zimepanda,"alisema.

### BODI ZA MISHAHARA

Hata hivyo, alisema ili kuendelea kulinda maslahi ya wafanyakazi anatambua jukumu la bodi za kima cha chini cha mishahara katika kuishauri serikali kuhusu upangaji wa kima cha chini cha mishahara pamoja na masharti mengine ya ajira katika sehemu za kazi.

"Serikali imeshaunda bodi za kima cha chini cha mshahara kwa sekta zote za umma na binafsi na tayari zimeanza kufanya tathmini ili kufanya maboresho ya kima cha chini cha mshahara kilichopo sasa,"alisema.

Aliagiza wizara zinazohusika na usimamizi wa bodi hizo kuhakikisha bodi zinawezeshwa ili kutekeleza majukumu yake kwa ufasaha na kwa lengo lililokusudiwa.

### KODI KWENYE MISHAHARA

Rais Samia alibainisha kuwa suala la kodi kwenye mishahara mwaka 2012 kiwango kilikuwa asilimia 18 lakini baada ya majadiliano kati ya serikali na vyama vya wafanyakazi kiwango kikashuka kwa asilimia tisa na kuanzia mwaka jana 2021 serikali ilipunguza hadi asilimia nane na kuongeza kiwango cha mshahara kinachokatwa kodi kutoka Sh.170,000 hadi 270,000.

Alisema pamoja na hatua hizo serikali imechukua hatua nyingine kadhaa za kuongeza pato la mfanyakazi.

"Mimi ni mama na mama ni mlezi ilinisukuma kuchukua hatua mwaka 2021, na kwa punguzo hilo la PAYE serikali haikukusanya Sh.bilioni 14.17, tuliongeza umri wa bima ya afya kutoka miaka 18 hadi 21, ambapo watoto zaidi ya 65,000 wamesajiliwa ambao kama wangelipiwa matibabu yao wazazi wangetoa Sh.bilioni 3.7 serikali imepokea mzigo, tozo ya asilimia sita ya mikopo elimu ya chuo kikuu na ya asilimia 10 ya adhabu ya kuchelewa kulipa, serikali imesamehe Sh.Bilioni 50 kwa mwaka mmoja,"alisema.

Pia alisema kwenye elimu ya juu kulikuwa na madeni chechefu ya Sh.Trilioni 1.1 yamefutwa na serikali.

"Tulipandisha vyeo wafanyakazi 198,215 ambapo Sh.bilioni 41 zimetumika kulipa mishahara yao mipya kutokana na kupanda vyeo, ubadilishaji wa kada watumishi 21,204 walinufaika na serikali ililipa Sh.bilioni 4.3, malimbikizo kwa watumishi 75,000 wamelipwa Sh.bilioni 124.3, ajira mpya Sh.bilioni 1.1, fedha zote zilibaki kwenu wafanyakazi tungetangaza kiwango cha mshahara wakati ule tukasema kima kadhaa kisingefikia fedha hizi,"alisema.

Alisema anaendelea kuyaangalia hayo katika mwaka ujao wa fedha huku ikikataa ombi la mikopo ya elimu ya juu kukatwa kwa asilimia nane na kusisitiza itabaki pale pale asilimia 15.

### MAFAO KWA WASTAAFU

Kuhusu mafao na nauli kwa wastaafu, Rais Samia aliagiza waajiri kuandaa malipo ya wastaafu wanaotarajiwa kabla ya tarehe ya kustaafu mtumishi.

"Kabla ya mtumishi kuondoka ofisini awe ameandaliwa stahiki zake zote na mafao yake yote na waajiri wahakikishe taarifa za watumishi wao zipo kikamilifu katika mifuko ya hifadhi ya jamii, kwa sababu kuna usumbufu mkubwa, naagiza ndani ya kipindi cha miezi sita ambacho mtumishi anatoa taarifa za kustaafu Maofisa Rasilimali watu wahakikishe wanaandaa stahili za mfanyakazi huyu, na mifuko ifanye uhakiki ndani ya muda huo,"alisema.

### UPANGAJI WA KIKOKOTOO

Rais Samia alisema "Nashukuru Katibu Mkuu TUCTA umekwenda hadi kutaja kiwango, tulikuwa tunavutana kutoka 25 kwenda 50 lakini leo TUCTA wamesema tukutane katikati sasa serikali tutakwenda kukaa katika utatu wetu na TUCTA kwa ajili ya kuangalia tutakavyofanya lakini wazo mlilokuja nalo siyo baya."

Aliomba TUCTA kutoa ushirikiano wa kutosha kwenye jambo hilo ili kwa mwaka huu suala la kikokotoo lifanikiwe na maslahi ya watumishi yapatikane kwa kiwango kinachomridhisha mtumishi.

Pia alisema serikali ipo kwenye hatua za mwisho kufanya tathmini ya uhai na uendelevu wa mifuko hadi Juni 30, mwaka 2021 ambapo yatatolewa mapendekezo ya namna bora ya kugharamia kundi la wastaafu bila kuathiri ustawi na uendelevu wa mifuko.

Kuhusu unyanyasaji, Rais Samia alionya matumizi mabaya ya sheria ya kuwaweka ndani watu kwa saa 48.

### NEEMA WATUMISHI LA 7

Rais Samia alitangaza neema kwa watumishi wa umma wa darasa la saba na waliondoshwa kwa vyeti feki.

"Nimepokea malalamiko ya TUCTA kuhusu darasa la saba ambao wameondoshwa pamoja na mkumbo wa vyeti feki, baada ya kikao changu na TUCTA na Mawaziri wanaohusika tulikaa kikao cha serikali peke yetu na tumewaza kuja na mambo yafuatayo kwamba waliofukuzwa waliofanya kazi kwa muda mrefu lakini wakafukuzwa kwa vyeti feki na kwamba hawakupata chochote cha kuondoka nacho nimewaagiza Wizara ya Utumishi pamoja na Wizara ya Fedha waangalie ni kiasi gani wafanyakazi wale walikatwa kwenye jasho la mishahara yao kile walichochangia kwenye mifuko walipwe,"alisema.

## TUCTA yawasilisha rasmi kwake kilio cha kikokotoo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SHIRIKISHO la Vyama Huru vya Wafanyakazi (TUCTA), limewasilisha mambo tisa kwa Rais Samia Suluhu Hassan ikiwamo kuongezwa kwa kiwango cha mkupuo wa pensheni(kikokotoo) kiwe kwa asilimia 33.

Akisoma risala ya wafanyakazi kwenye sherehe za Mei mosi mwaka 2022, Katibu Mkuu wa TUCTA, Henry Mkunda,alisema shirikisho hilo linafahamu mchakato wa upatikanaji wa kikokotoo bora cha mafao kwa wastaafu unaendelea na imekuwa ikishirikishwa na serikali kila hatua.

"Pamoja na kushirikishwa uandaaji wa kanuni mpya za mafao ya pensheni, tunapendekeza kuongezwa kiwango cha mkupuo wa kiwango cha pensheni kutoka asilimia 25 iliyokataliwa awali angalau ifikie asilimia 33, tumeomba pia serikali iridhie mapema mapendekezo ya kanuni iliyopendekezwa na kamati ya uongozi,"alisema.

Kuhusu kima cha chini cha mshahara kwa sekta zote za umma na binafsi, alisema wafanyakazi hawajaongezewa mishahara kwa takribani miaka tisa kwa sekta binafsi na miaka saba kwa sekta ya umma hali hiyo imesababisha kupungua kwa ari ya kufanya kazi hivyo kupunguza ufanisi na uwajibikaji na tija mahali pa kazi.

Mkunda alisema ni wazi gharama za maisha zimezidi kupanda na ilihali stahiki na ujira wa wafanyakazi umeendelea kuwa duni na kubainisha kuwa kwa sasa mshahara wa kima cha chini kwa sekta binafsi ni kati ya Sh.40,000 hadi Sh.60,000 kwa mfanyakazi wa majumbani.

Aidha, alisema kwa wafanyakazi wa mashambani na viwandani ni Sh.100,000 , viwango vilivyotangazwa mwaka 2013 katika gazeti la Serikali na kwa upande wa wafanyakazi wa umma, kima cha chini cha mishahara ni Sh. 300,000 kilichotangazwa mwaka 2015.

"Kufuatia hali hiyo, TUCTA ilifanya utafiti mwaka 2006 na kuwasilisha mapendekezo serikalini mapendekezo kuwa kima cha chini cha mshahara kinachomwezesha mfanyakazi kumudu mahitaji muhimu kwa wakati huo Sh.315,000 ingetosha kumudu gharama za maisha."

"TUCTA ilifanya utafiti mwingine mwaka 2014 na kubaini kuwa malipo ya mishahara ya Sh.720,000 kwa mwezi yangemwezesha mfanyakazi wa kima cha chini kumudu gharama za maisha,"alisema.

Alisema pamoja na mapendekezo hayo viwango hivyo havijakubaliwa na Serikali na kwamba kutokubaliwa kwa mapendekezo hayo kumeathiri wafanyakazi na familia zao kutokana kupanda kwa gharama za maisha na kuwafanya kuishi maisha ya chini ya mstari wa umasikini.

Pia alisema bado wana kilio cha kodi kwenye marupurupu mengine na kuomba wakiangalie zaidi itasaidia kupunguza makali ya maisha.

Kuhusu Bima ya Afya, aliomba waangalie gharama za baadhi ya magonjwa makubwa na kuwawezesha sekta binafsi kupata huduma ya matibabu hata baada ya kustaafu.


Alilalamikia kitendo cha wafanyakazi kuendelea kufanya kazi kwa mikataba kwa muda mrefu bila ya kupewa ajira.

Rais wa TUCTA, Tumaini Nyamhokya, aliomba kasi ya kuwarejesha kazini watumishi waliokuwa na elimu ya darasa la saba ambao waliondolewa kazini lakini wamesoma na kuhitimu kidato cha nne iongezwe na wale ambao walikuwa wamefikia umri wa kustaafu wapewe mafao yao ili yawasaidie.

Aidha, aliomba bodi ya mishahara ya sekta binafsi ikae kwa haraka ili na watu wa sekta hiyo nao wapandishiwe kima cha chini cha mishahara.

Mwenyekiti wa Chama cha Waajiri Nchini (ATE), Jayne Nyimbo, alisema kuna mlundikano wa kodi zinazotozwa nchini ambazo zimeongeza gharama kwa waajiri.

## KUMBUKUMBU



# DR. REGINALD MENGI

29TH MEI, 1942 - 2ND MEI, 2019

## Hakika Ameacha Alama

IPP
Cares For You

# NECTA kuanza kusahihisha mitihani kidijitali mwezi huu

**Na Christina Mwakangale**



Ofisa Uhusiano wa Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), John Nchimbi akizungumza na mwandishi wetu. **PICHA: NIPASHE DIGITAL**

MFUMO mpya wa usahihishaji mitihani kidijitali unaosimamiwa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), kwa watahiniwa wa shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu unatarajiwa kuanza kazi kwa mara ya kwanza mwaka huu, ukianza na mitihani ya walimu, inayofanyika wiki ijayo.

Matumizi ya teknolojia ya kielektroniki kusahihisha yataokoa fedha, muda na kuongeza ufanisi, Ofisa Habari na Uhusiano NECTA, John Nchimbi, anasema katika mahojiano maalum na Nipashe.

Majaribio ya matumizi ya mfumo huo yamekwishafanyika kwenye vyuo vyote vya ualimu nchini, kujiandaa na usahihishaji kidijitali ambao unaanzia mitihani ya watahiniwa wa ngazi ya cheti na diploma ya ualimu, inayotarajia kuanza wiki Ijayo Mei 9, 2022.

Katika mahojiano hayo yaliyofanyika Dar es Salaam, Nchimbi anasema NECTA imepanga kuwa ifikapo 2025 usahihishaji kidijitali utafanywa kwa mitihani yote ikiwamo ya darasa la nne na ya kumaliza elimu ya msingi, kidato cha pili, cha nne, sita na ya ualimu.

**Endelea na Mahojiano.....**

**SWALI:** Unaweza kutufafanulia zaidi kuhusu mfumo wa usahihishaji mitihani uliozinduliwa hivi karibuni na NECTA?**JIBU:** Ili kuufahamu mfumo mpya wa kidigitali, nizungumzie wa kianalojia uliotumika kwa miongo mingi.

Baraza tunavyosahihisha mitihani kwa sasa tunawatumia watahini au wasahihishaji kutoka sehemu mbalimbali nchi nzima.

Mfano, mtihani wa kidato cha nne tunaweza kuwa na vituo kama nane vya kazi, mtihani wa hisabati unaweza ukasahihishwa Dar es Salaam, Fizikia Kigoma, Kemia Morogoro na sehemu nyingine mbalimbali. Hawa watahini wakiitwa kwenye kituo cha usahihishaji wanakaa kwenye jopo mtihani mmoja, jopo linaweza kuwa na maswali saba, nane hata 10, kila msahihishaji anapewa swali lake.

Tunaita mnyororo wa usahihishaji unaozunguka kutoka swali la kwanza hadi la mwisho kila mmoja kwa swali lake. Mtihani ukishasahihishwa unakwenda kwa mhakiki kuhakikisha usawa wa kile kilichosahihishwa, akiona kimekaa sawa ataupeleka kwa mtu anayeingiza alama kwenye kompyuta.

Hatua nyingine hufuata, kwa kifupi usahihishaji mtihani wa kitaifa unazingatia vitu vingi kwa wanajopo. Mfumo huu wa analojia unatumiwa na nchi mbalimbali na wengine walikuja kujifunza kwetu.

Tofauti na mitihani ya kawaida mwalimu wa somo fulani atasahihisha somo hilo hilo maswali yote, hii inamchosha na pia ufanisi unapungua.

Sasa tunaingia kwenye kusahihisha kidijitali au kielektroniki 'electronic marking' na mwaka huu unaanzia mitihani ya ualimu. Mfumo hautowalazimu watahini kukutana kwenye kituo cha usahihishaji.

Badala ya kukusanya watu, watakaa pale walipo wanapofanyia kazi ila wanapaswa wawe na kompyuta.

Msahihishaji atapewa nywila au neno la siri (password) na NECTA , atasubiri muda ukifika akifungua kompyuta mfumo utakuja. Badala ya kuwa na karatasi za mitahani, kalamu nyekundu kama zamani, sasa atatumia 'mouse' au kipanya. Mfumo unabainisha jibu hili lina alama kadhaa kulingana na mwongozo wa usahihishaji.

**SWALI:** Kabla ya kusahihisha maswali msahihishaji anayaona kwenye kompyuta? Mfano, mtihani una maswali 20, naye anatakiwa kusahihisha swali moja, Je, atayaona yote au lile linalomhusu?

**JIBU:** Mtu anayesahihisha anaona swali lake tu. Akisha 'save' swali linaondoka, linakuja la mwanafunzi au mtahiniwa mwingine ila ni lilelile moja linalomhusu.

**SWALI:** Mitihani ipi itahusika?

**JIBU:** NECTA tunahusika na mtihani wa darasa la nne, la saba, kidato cha nne, sita, walimu ngazi ya cheti na diploma. Usahihishaji wa kidijitali kwa mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi, mwaka 2012 wanafunzi wakianza kufanya mtihani kwa kutumia karatasi za OMR (Optical Mark Reader), mtihani ulijibiwa kwa maswali ya kuchagua, mashine iliskani mtihani uliojibiwa na kusahihisha.

Mfumo ukabadilika baadaye maswali badala ya kuwa ya kuchagua yote, ikawa 40 ya kuchagua na matano ya kujibu kwa kuandika au kufanya mahesabu. Hivyo 40 yalisahihishwa kwa 'scanner' na haya matano ilimlazimu msahihishaji atumie kalamu.

Ila mwaka jana tukasema hapana, haya maswali yote yaingizwe katika mfumo wa kidijitali. Mwaka huu mitihani ya walimu itasahihishiwa kidijitali.

Mwakani tunatarajia kidato cha sita usahihishwe kidijitali na 2024 utakuwa wa kidato cha pili na 2025 utakuwa wa sekondari.

**SWALI:** Matumizi ya teknolojia yatarahisisha kazi na kupunguza muda wa kazi, ingawa mijadala kwenye jamii ni kuhusu maswali ya kujieleza hujibiwa kwa uelewa tofauti, inakuwaje kwenye kutoa alama?

**JIBU :** Ili mtu aelewe usahihishaji kidijitali ni lazima auelewe huu wa analojia ambao tumeutumia hapo awali. Jamii ijue kabla usahihishaji haujaanza huwapo majadiliano, kwamba swali la kwanza lina alama tano, mtu akipewa swali la kujieleza atatumia mwongozo na uzoefu wa kazi ya usahihishaji kulingana na anavyoliona kwenye kompyuta.

Mtahini au msahihishaji atasahihisha kulingana na mwongozo. Kilichobadilika ni kwamba mfumo huu hautumii kalamu, hauwakusanyi wasahihishaji ila mtu atatumia kompyuta na kuliona swali na jibu la mtahiniwa na kutoa alama.

Watanzania waondoe hofu kuhusu usahishaji kidijitali.

**SWALI:** Baada ya majibu kutunzwa kwenye kompyuta au kidijitali hakuna changamoto au hatari ya kufanyiwa udukuzi kwenye mfumo na kupoteza ya mitihani ya nchi nzima?

**SWALI:** Mifumo hii imeundwa na wataalamu IT wa NECTA, unaweza ukaingiliwa lakini ni rahisi kupata (recover), tumeweka vidhibiti, ili iwe rahisi kwa wataalamu wetu kudhibiti.

**SWALI:** Vipi kuhusu kompyuta za usahihishaji ni za kutosha?

**JIBU:** Sehemu ziliko na vituo vya usahihishaji kuna kompyuta na pia baraza tumejipanga. Tutaifanya kazi hii kwa ifanisi.

Aprili 20, mwaka huu vyuo vyote vya ualimu yamefanyika majaribio ili kujiridhisha iwapo mfumo huu utafanikiwa.

Mfano tu, kuanzia mwaka 2020 tulianza kutumia karatasi za OMR, ambazo ni maalum kwa kufanyiwa 'scanning' katika kompyuta, zinazotengezwa ndani ya nchi, wakati wa corona ulitufunza kujiongeza na kufikiri kujitegemea.

**SWALI:** Ni yepi manufaa ya mfumo huu, kiuchumi?


**JIBU:** Nitoe mfano tu mtihani wa kidato cha nne, cha pili na darasa la nne mwaka jana kazi ya kusafirisha watahini au wasahihishaji 28,000 tulitumia milioni 500 ambao walitoka maeneo yao hadi kituo cha usahihshaji, chakula kiligharimu bilioni tisa hapo hujaweka posho.

Mwaka huu ambao watasahihisha mitihani ya walimu tutaokoa Sh. milioni 550. Kuna ongezeko la watahiniwa baada ya sera ya elimu bure.

Kwa hiyo mfumo huu utarahisisha kazi. Tunahamasishwa kutumia TEHAMA kufanya kazi kwa ufanisi na kuokoa pesa ili kuongeza ufanisi na tija.

Kwa mfumo huu tutahakikisha mtahiniwa haki yake inapatikana, haya ni maisha.


## KUPOTEA KWA CHETI



116837502

**CALEB NATHANAEL JOHN** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato che nne chenye index namba **S.1601-0021** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **TENGERU BOYS SEKONDARI** mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/KIJ/RB/511430/2021.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya MOROGORO**

**Kituo cha MJINI Mkoa Wa MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na...... 20......2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU PETER EMANUEL KAVISHE WA MAFISA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA GODFREY PETER KAVISHE AMAPUNDA**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

116837602

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 16 Mwezi 5 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

**Imetolewa Tarehe 25 Mwezi 04 Mwaka 2022.**

## TANGAZO



**HADIJA HAMASI MZEE**

116838802

**MIMI HADIJA HAMASI MZEE** natangaza kubadili jina langu kutoka **HADIJA HAMASI JONGO** kama lilivyosajiliwa kwenye kitambulisho changu cha **NIDA** na kuwa **HADIJA HAMASI MZEE** kwa ajili ya matumizi yangu kwenye taasisi mbalimbali za selikali na binafsi.

**Ref.RD|OPT|MG|2022|11|113** kutoka Ministry of Lands and Human Settlements Development.

Yeyote mwenye pingamizi na hili basi atoe taarifa kupitia kituo cha polisi kilicho karibu na yeye.

ENCLOSURES:

Sir/Madam/Gentlemen, Your Obedient Servant,

Asst.Registrar of Titles



Mbunge wa jimbo la Ubungo, Prof Kitila Mkumbo, (wa pili kushoto) akiwa na Diwani wa kata ya Kimara, Ismali Mvugi,(wapili kulia) katika eneo la Mavurunza Wilaya ya Ubungo mkoani Dar es Salaam jana, walipofanya ziara ya kukagua miradi ya barabara iliyotekelezwa kwa fedha za mfuko wa jimbo.PICHA: MIRAJI MSALA

# Serikali yafuta leseni 200 za uchimbaji

**Na Gwamaka Alipipi,**
DODOMA

SERIKALI imefuta leseni 200 za uchimbaji wa madini ambazo wamiliki wake wameshindwa kuzifanyia utafiti na kuanza uchimbaji, huku taratibu za kufuta zingine 400 zikiendelea.

Waziri wa Madini, Doto Biteko, alitoa takwimu hizo mwishoni mwa wiki bungeni wakati akijibu hoja za wabunge kwenye hitimisho la hoja yake ya kuomba makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2022/23.

Waziri Biteko alisema kuna maeneo wafanyabiashara walipewa leseni za uchimbaji madini lakini hawajafanya lolote kwa miaka mingi kwa mtazamo wa macho. Waziri Biteko alisema: "Nataka kuwahakikishia kwamba Wizara ya Madini tangu tumeanza kuwapa nguvu wachimbaji wadogo tunapata lawama sana kwamba tunafuta leseni, lakini sisi tunatekeleza maelekezo ya Bunge na viongozi wetu."

Aliongeza: "Hadi sasa tumeshafuta leseni zaidi ya 200 ambazo ni domant (mfu), zipo nyingine nyingi zaidi ya 400 ambazo process (mchakato) wa kuzifuta unaendelea. "Process (mchakato) wa kufuta leseni una lawama nyingi, sisi Wizara ya Madini tumekubali kubeba lawama kwa niaba ya wachimbaji wadogo."

Waziri Biteko alisema kuna wachimbaji madini wenye tabia ya kushika maeneo kwa maana ya udalali, wanategeshea kuona nani anakuja , wengine wanasubiri hadi wachimbaji wadogo waje kuchimba ndipo anajitokeza na kuwaambia hili ni eneo langu na kuanza kuwafukuza.

"Naomba niwaambie wachimbaji wakubwa wa madini wanaotekeleza sheria tutawalinda lakini wale ambao hawatekelezi sheria maeneo yao tutayachukua na kuwapatia wale ambao wanahitaji kufanya uchimbaji," alisema Waziri Biteko.

Hata hivyo, alisema katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi, 2022, Tume ya Madini imetoa leseni 8,172 za uchimbaji madini ikilinganishwa na leseni 6,314 katika kipindi kama hicho mwaka 2020/2021, sawa na ongezeko la asilimia 17.3.

Alisema leseni hizo zinajumuisha leseni mbili za uchimbaji mkubwa, leseni tano za uchimbaji wa kati, leseni 282 za utafutaji wa madini, leseni 5,937 za uchimbaji mdogo, leseni 49 za uchenjuaji wa madini, leseni mbili za usafishaji wa madini na leseni 1,895 za biashara ya madini.

Aidha, akitaja vipaumbele vya wizara yake kwa mwaka wa fedha 2022/23, Waziri Biteko alisema wataendelea kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa sekta ya madini kwenye pato la taifa.

Alisema pia wizara yake itawaendeleza wachimbaji wadogo na kuwawezesha wananchi kushiriki katika uchumi wa madini, kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini.

Kipaumbele kingine ni kuhamasisha biashara na uwekezaji katika sekta ya madini, kusimamia mfumo wa ukaguzi wa shughuli za migodi, kuzijengea uwezo taasisi zilizo chini ya wizara ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi, kuendeleza rasilimali watu na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.

# Jaji Mutunga atunga kitabu cha maisha ya ujaji mkuu

**Na Joseph Mwendapole**

JAJI Mkuu mstaafu wa Kenya, Willy Mutunga ameandika kitabu kuhusu aliyoyapitia akiwa kwenye nafasi hiyo huku akiwataka watanzania kukisoma ili wapate mambo yatakayowasaidia kudai Katiba mpya.

Jaji Mutuga kwenye kitabu hicho ameelezea mchakato wote uliofanyika hadi nchi hiyo kufanikiwa kuwa na Mahakama Huru ambayo haiingiliwi na mhimili wowote kwenye kufanya maamuzi yake.

Aliyasema hayo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa kitabu hicho alichokipa jina la Beacons of Judiciary Transformation, ambapo mgeni rasmi alikuwa Jaji Mkuu mstaafu wa Tanzania, Othman Chande.

Jaji Mutunga alikuwa Jaji Mkuu wa Kenya kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2011 mpaka 2016 na atakumbukwa na wakenya alivyoifanya Mahakama nchini humo kuwa huru katika maamuzi yake. "Tanzania mnapambania katiba mpya na kuna ile rasimu ya Katiba ya Warioba kwa hiyo naona hiki kitabu kitawasaidia kwenye hayo mapambano kwa sababu kina mambo mengi kuhusu katiba mpya. Kitabu kinazungumzia shida za kupata hiyo katiba mpya na namna ya kuitekeleza," alisema Jaji Mutunga.

Hata hivyo, Jaji Mutunga alisema kupata Katiba mpya ni kitu kingine na kuitekeleza ni kitu kingine kwani kwenye baadhi ya nchi uzoefu unaonyesha kuwa uzingatiaji wa Katiba unategemea matakwa ya Rais aliyeko madarakani.

"Kutekeleza Katiba kwenye baadhi ya nchi inakuwa ni mapambano mengine, Katiba ni nyaraka tu hivyo kuitekeleza kunaweza kuleta shida sana na mfano mzuri wa kiongozi wa kuigwa kwenye kutekeleza Katiba ni Mwalimu Julius Nyerere, lakini wengine ni shida sana," alisema Mutunga

Kwa upande wake, Jaji Mkuu mstaafu, Othman Chande, alisema kitabu hicho nikumbukumbu ya hotuba 60 na maamuzi yake saba aliyoyatoa akiwa kwenye nafasi ya Jaji Mkuu wa Kenya kwa miaka mitano.

Alisema kwenye kitabu hicho Mutunga amejikita zaidi kwenye mageuzi ya mahakama ambapo baada ya kupata Katiba mpya mwaka 2010, wakenya wengi walitaka mahakimu na majaji wote afukuzwe kazi mahakama zote zifutwe waanze upya.

"Wakenya si kwamba tu walitaka Katiba mpya bali na mahakama mpya na yeye Mutunga ndiye alikuwa Jaji Mkuu wa kwanza ndani ya Katiba mpya ya Kenya alifanya mageuzi makubwa sana," alisema

Aidha, alisema Mutunga aliwezesha mahakama kuwa huru kutoingiliwa na mhimili mwingine na alikuwa Mwenyekiti wa Jopo la Majaji sita kwenye kesi ya kwanza ya uchaguzi wa urais mwaka 2013.

"Amezungumzia uzoefu wake kwenye hali kama hiyo, anasema katika kutoa uamuzi wa kesi za urais mara zote utafurahisha watu wa upande mmoja na utawaudhi watu upande mwingine lakini unapaswa kutoa uamuzi wa haki, " alisema

"Kwenye ile kesi aliamua kwamba Uhuru ndiye mshindi ingawa kuna watu walikuwa na matarajio mengine na walimuona kama adui, lakini cha kutia moyo ni kwamba mwenyewe amesema kuwa wakati anamuapisha Uhuru Kenyatta alishangiliwa yeye zaidi wakati anaingia uwanjani kuliko hata huyo Rais mwenyewe," alisema Chande.

# NGO zaombwa kutoa elimu sensa ya watu na makazi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imetoa wito kwa mashirika yote yasiyo ya kiserikali (NGOs) kushirikiana na serikali kutoa elimu kuhusu umuhimu wa sensa ya watu na makazi ili jamii ishiriki kikamilifu.

Kauli hiyo ilitolewa jijini Dar es Salaam na Msajili wa NGOs kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Vickness Mayao, wakati wa uzinduzi wa mradi wa DigitalNGO ambao unatarajiwa kuwa kichocheo cha mabadiliko na mapokeo ya kidijitali kwa mashirika yasiyo ya kiserikali nchini Tanzania.

Alisema katika kipindi hiki cha kuelekea katika sensa wanatambua kuwa NGOs zina mchango mkubwa katika jamii na wanazihimiza kutoa elimu nzuri ili watu wengi waone umuhimu wa kushiriki na kujitokeza kuhesabiwa.

Akizindua mradi huo, pia alizitaka NGOs hizo kuona umuhimu wa kuweka taarifa zao katika mifumo ya kidijitali badala ya kwenye vitabu au karatasi kama wanavyofanya sasa.

Mayao alisema serikali inataka kuona kila taasisi na mashirika yanatoka katika matumizi ya karatasi na kutumia mfumo wa kidijitali.

"Tunafahamu kuwa mashirika haya yakiwa na mifumo ambayo wameitengeneza wenyewe itawasaidia kuitumia katika utekelezaji wa majukumu yao hata kwa serikali itakuwa rahisi kupata data kwa usahihi na kujua mchango wa NGOs hizo katika maendeleo ya nchi," alisema Mayao.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Taasisi ya Media Convergency ambao ndiyo wasimamizi wa mradi huo, Asha Abinallah, alisema lengo ni kuziwezesha NGOs zifanye kazi kuendana na kasi ya kidjitali.

"Na tutajikita katika maeneo muhimu manne na tutaanza na NGOs 35 ambazo zitaonyesha utayari," alisema Abinallah.

Alisema pia kupitia mradi huo watafanya mafunzo na umelenga kuwafikia watu 1000 kila baada ya wiki mbili mpaka tatu ili kuhakikisha wamekuza uelewa kwa NGOs hizo kujiendesha kidijitali.

"Pia tutajitahidi kadiri ya uwezo wetu kutoa taarifa zinazohusiana na mapungufu yaliyopo katika ujuzi wa kidijitali kwenye mashirika yasiyo ya kiserikali pamoja na kuwaambia watu fursa zilizopo katika eneo hili," alisema Abinallah.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa TEHAMA kutoka Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mulembwa Munaku, alisema matumizi ya teknolojia ni muhimu na watahakikisha wanawaunga mkono kufanikisha kazi hiyo waiyoianza.

"Maana yake taasisi zote za ndani ya nchi ziwe za serikali au binafsi zijenge utaratibu wa kutumia teknolojia ya TEHAMA katika kufanya shughuli zao ikiwamo kutoa huduma kwa wateja wao," alisema Munaku.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bingwa Ligi Kuu Bara, vita nne-bora bado, TFF isilale

**JUMAMOSI** tumeshuhudia 'dabi' ya watani wa jadi, Simba na Yanga, ikipigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa na kumalizika kwa sare ya bila kufunga, matokeo hayo yakifanana na yale ya mzunguko wa kwanza, hivyo kufanya miamba hiyo kushindwa kutambiana katika Ligi Kuu msimu huu wa 2021/22.

Hata hivyo, mechi hiyo ilikuwa ikitarajiwa kupunguza mbio za Yanga kuelekea kuwania kutwaa ubingwa msimu huu kama Simba ingeshinda, lakini bado matokeo hayo hajahalalisha moja kwa moja vinara hao wa Ligi Kuu Bara kujihakikishia kutwaa taji hilo kwa mara ya kwanza baada ya misimu minne. Licha Yanga kuwa na pointi 55 kileleni, 13 zaidi ya Simba iliyopo nafasi ya pili huku zikiwa zimebaki takriban mechi tisa kabla Ligi hiyo kumalizika msimu huu, kimahesabu bado ligi haijamalizika hadi itafikia ukingoni kwani lolote linaweza kutokea ingawa kwa muonekano ni vigumu.

Yanga imebakiza mechi tisa wakati Simba imebakiza mechi 10 kabla ya ligi hiyo kumalizika, hivyo ili Simba iwe bingwa inahitaji kushinda mechi zake zote zitakazoiwezesha kumaliza na pointi 72 wakati huo ikiombea Yanga kupoteza pointi 11 katika michezo yake tisa iyobaki jambo ambalo ni vigumu, lakini kwenye soka lolote linaweza kutokea.

Pamoja na vita hivyo, vya kuwania ubingwa ambavyo vinaonekana kuwa upande wa Yanga kama itachanga karata zake vema kwa kushinda mechi sita tu kati ya tisa, bado kuna mpambano mkali kwa upande wa kuwania nafasi nne za juu katika ligi hiyo ambayo msimu huu kuna bonasi kubwa kutoka kwa wadhamini wa haki za matangazo ya televisheni, Kampuni ya Azam Media Limited.

Ushindani huo umeongezeka kutokana na Kampuni ya Azam Media Limited kutangaza bonasi kubwa katika mkataba wa udhanimi walioingia na Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB) na Shirikisho la Soka nchini Mei mwaka jana wenye thamani ya Sh. bilioni 225.6 kwa kipindi cha miaka 10.

Katika mkataba huo bingwa atapata mbali na zawadi kutoka kwa mdhamini mkuu, Benki ya NBC, Azam Media Ltd itatoa bonasi ya Sh. milioni 500, mshindi wa pili milioni 250, watatu milioni 225, wa nne milioni 200 na zitakwenda zikipungua hadi timu zitakazocheza mechi ya mtoano kuwania kucheza Ligi Kuu msimu ujao, zikilamba milioni 20 kila moja.

Lakini pia juhudi za Simba kufanya vizuri kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika kwa kufika hatua ya robo fainali, kumeiongezea Tanzania pointi na kuwa miongoni mwa nchi 12 zitakazoingiza timu nne kwenye michuano ya kimataifa; mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho. Kwa mantiki hiyo, kuna uwezekano mkubwa timu zitakazomaliza nafasi nne za juu msimu huu zikakata tiketi moja kwa moja kushiriki michuano hiyo yenye utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika, jambo ambalo limezidi kuongeza ushindani mkubwa katika ligi hiyo. Hiyo ni kutokana na msimu huu kuwapo kwa uwezekano mkubwa kwa Simba ama Yanga kucheza fainali ya Kombe la Shirikisho la Soka nchini maarufu FA Cup na dhidi ya Azam FC ama Coastal Union, hivyo moja kati ya watani hao wa jadi wakibeba ubingwa, tiketi ya kucheza Kombe la Shirikisho Afrika itarudi kwenye timu zilizomaliza nafasi nne za juu Ligi Kuu Bara.

Jambo ambalo linaweza kutokea, lakini pia kama Coastal Union ama Azam FC mojawapo itatwaa Kombe la FA, basi timu tatu zitakazomaliza nafasi ya juu kwenye Ligi Kuu zitakata tiketi ya kucheza michuano ya kimataifa pamoja na iliyobeba ubingwa huo wa FA.

Kutokana na vita hivyo, kuna haja kwa TFF na TPLB, kuelekeza macho yao kwenye hatua hii ya lala salama Ligi Kuu Bara, kwani kunaweza kuchezeka mchezo mchafu wa rushwa ili kupanga matokeo kuanzia vita vya ubingwa hadi zinazowania kumaliza nafasi ya tatu na ya nne.

Lakini pia ikumbukwe kuna kundi linalopambana kuepuka kwenda kucheza mechi za mchujo na timu mbili kutoka Ligi ya Championship, ili kucheza Ligi Kuu msimu ujao, hivyo nako si salama hasa ukizingatia timu zote ukiondoa Simba na Yanga, zilizobaki nyingi zinapishana pointi moja hadi tatu tu kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Hivyo, tunaitaka TFF na TPLB kuongeza umakini na ikiwezekana kuvishiriksiha vyombo vya usalama na zaidi Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), ili kuzuia upangaji wa matokeo ambao utakwenda kusababisha kupatikana wawakilishi wabovu kwenye michuano ya kimataifa msimu ujao, lakini pia ukipora haki ya timu zinazostahili bonasi kubwa kutoka kwa wadhamini na zile zitakazopoteza haki yao ya kuendelea kuwamo Ligi Kuu msimu ujao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

Na Adam Fungamwango

# Taratibu wageni wanaanza kuiteka 'dabi' Simba, Yanga

**ILIKUWA** ni kawaida miaka kadhaa nyuma kusikia majina ya wachezaji wa Kitanzania yakitajwa mara baada ya mechi za watani wa jadi, Simba na Yanga kumalizika.

Hata kama wageni walikuwapo, lakini ni Watanzania ndiyo kwa kiasi kikubwa walionekana kucheza kwa kujituma na kupambana kwa sababu wao ndiyo wanaojua homa ya 'dabi' ya Simba na Yanga inavyokuwa huko mitaani tofauti na wageni.

Mara nyingi wageni wanakuwa wanahadithiwa tu namna watu wanavyoichukulia mechi hiyo, na kama watawaona mashabiki wanavyokuwa huko mitaani, lakini si kama wachezaji ambao wamezaliwa na kukulia kwenye maisha hayo.

Ndiyo maana huko nyuma tuliona wachezaji wa Kitanzania walivyokuwa wakipambana kufa au kupona, na kucheza kwa kujitoa mara mbili tofauti na inavyokuwa kwenye mechi za kawaida, kiasi cha kuwashangaza hata wageni.

Tunawakumbuka wachezaji kama kina Sunday Manara, Kitwana Manara, Gibson Sembuli, Juma Mkambi wa Yanga na Abdallah Kibadeni, Adam Sabu, Abdallah Mwinyimkuu, Thuwen Ally wa Simba miaka ya 1970 hadi mwanzoni mwa 1980 walivyoipamba 'dabi'.

Kuanzia miaka ya 1980 walikuja kina Omari Hussein, Rashid Hanzuruni, Makumbi Juma, Sanifu Lazaro kwa upande wa Yanga na kina Zamoyoni Mogella, Edward Chumila, Malota Soma kwa upande wa Simba.

Mwanzoni mwa miaka ya 1990, ndipo walipoanza kuja wageni kama kina Damin Kimti, William Fuhnbulleh, Contastine Kimanda na kuwika, lakini bado walikutana na upinzani mkali wa wenye 'dabi' wenyewe kina Sekilojo Chambua, Edgar Fongo, na wengine wengi kwa upande wa Yanga, huku Simba ikiwa na kina Nteze John, John Makelele na wengine wengi.

Hata miaka ya 2000, walipokuja wageni kama kina Emmanuel Okwi, Hamisi Kiiza, Didier Kavumbagu, Haruna Niyonzima na marehemu Patrick Mafisango, ambao ndiyo kwa kiasi kikubwa walioanza kuleta mapinduzi ya wachezaji kutoka nje, kung'ara kwenye dabi, lakini bado pia walikutana na upinzani mkali kutoka kwa kina Jonas Mkude, William Lucian 'Gallas', Haruna Chanongo, Salum Athumani, Kudra Omari, Ibrahim Ajibu, Shiza Kichuya, Mrisho Ngasa na wengine wengi.

Hawa ni wachezaji ambao wanaijua 'dabi' toka bado wadogo kule mitaani. Na wanajua jinsi mashabiki wanavyotaniana, wanavyoteseka, na wanavyoichukulia timu moja inaposhinda au kufungwa, ndiyo maana na wao wanachukua hisia wanazozipata mitaani wanazipeka uwanjani. Kwa sasa naona jambo hili linaanza kupungua kwa kiasi kikubwa. Wachezaji wa kigeni sasa ndiyo kama vile wanaonekana kuanza kujua thamani ya 'dabi' kuliko wenyeji wenyewe.

Jumamosi iliyopita tuliona wachezaji wachache tu walioonekana kucheza kama 'dabi', huku wengine hasa Watanzania wakicheza kama mechi nyingine tu ya Ligi Kuu.

Wachezaji kama Fiston Mayele na Henoc Inonga ambao ni Wakongomani, wameonekana kuitawala 'dabi' hiyo na kufanya vitu ambavyo vilikuwa vikiwafurahisha mashabiki waliokuwapo uwanjani na waliokuwa wakiangalia televisheni.

Walicheza hasa 'kidabidabi', Mayele akitafuta nafasi kwa kila hali ili afunge bao, lakini Inonga akitibua kila jaribio lake la kutaka kufunga na hii ndiyo iliyokuwa burudani kubwa waliyoipata mashabiki, kwani mechi yenyewe haikuwa na mashambulizi ambayo yangeweza kuwafanya wasimame vitini na kushangilia. Mchezaji pekee wa Kibongo aliyeonekana kuitendea haki 'dabi' ni Kibwana Shomari, kwani uchezaji wake uliakisi aina ya mechi yenyewe alivyokuwa akicheza kwa kujituma na kwa kiwango cha hali ya juu.

Tunajua kuwa ni kweli kwa sasa timu za Simba na Yanga zina wachezaji wengi wa kigeni, huku ikiruhusiwa kila timu kusajili nyota 12 kutoka nje ya nchi, lakini inaonekana ni kama vile wachezaji wa Kitanzania wamekuwa ama hawajitumi kwenye 'dabi' hiyo au kwa miaka ya karibuni wamezidiwa sana viwango na wachezaji wa kigeni.

Hii ni kengele ya hatari kuwa huko tuendako, dabi zote zikiisha watakuwa wakizungumzwa wachezaji wa kigeni jinsi walivyong'ara. Na hii si dhambi, kama wao ndiyo wanaona umuhimu wa mchezo huo tofauti na Watanzania kwa nini wasisifiwe?

Kinachotakiwa sasa ni wachezaji wa Kitanzania kuanza kujitazama upya kupitia mchezo huu. Wachezaji wengi wa zamani hupata jina, sifa na kujulikana nchini kupitia michezo kama hii, hivyo hujituma sana linapokuja suala la mechi ya Simba na Yanga.

Mchezaji wa Kitanzania anayecheza mechi ya Simba na Yanga kama anacheza mechi nyingine tu ya Ligi Kuu, basi ataendelea kuwa vile vile tu.

HABARI KITAIFA

# Wafanyakazi walipwa bil. 8/- madai mbalimbali

**Na Richard Makore,**
MWANZA

SERIKALI mkoani Mwanza imetumia zaidi ya Shilingi bilioni nane kulipa madai mbalimbali ya wafanyakazi wake katika kipindi cha mwaka mmoja.

Kauli hiyo ilitolewa jana jijini Mwanza katika Sherehe ya Siku ya Wafanyakazi iliyofanyika kimkoa uwanja wa CCM Kirumba, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, alisema serikali imeendelea kuthamini mchango wa wafanyakazi wote wakiwamo wa sekta binafsi na umma katika kukuza uchumi wa nchi.

Alisema serikali imelipa zaidi ya Sh. bilioni 5.2 kama malimbikizo ya mishahara kwa watumishi wa umma pamoja malipo ya zaidi ya Shilingi bilioni tatu mkoani humo ambazo sio mishahara.

Pia, katika kipindi cha awamu ya sita ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, serikali imepandisha watumishi wake madaraja mkoani humo na kuanza kulipa mishahara mipya.

Alisema wafanyakazi ni nguzo muhimu katika kujenga uchumi wa nchi na itaendelea kusimamia suala la uboreshaji wa maslahi yao katika sekta zote.

Aliwataka waajiri wote mkoani Mwanza kulipa mishahara ya wafanyakazi wao kwa wakati kama Sheria ya Ajira inavyotaka.

Aliwakumbusha waajiri kulipa makato ya kila mwezi ya wafanyakazi yanayotakiwa kupeleka katika mifuko ya hifadhi ya jamii.

Alisema kwa kuwa hivi sasa dunia imekuwa ya kidijitali inatakiwa mifuko ya hifadhi za jamii kuweka mifumo ambayo inaweza kumpa fursa mfanyakakazi kuangalia michango yake kupitia simu ya mkononi.

Kwa upande wake, Mratibu wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA), mkoani Mwanza, Zebedayo Athuman, aliwataka waajiri kuweka mbele maslahi ya wafanyakazi na kuyalinda.

Alisema waajiri wengi wamekuwa wakiukaji wa haki hizo, licha ya sheria ya ajira kuwapo na kwamba wao kama shirikisho wataendelea kupaza sauti zao katika suala hilo. Kaulimbiu ya Siku ya Wafanyakazi inasema, 'Mishahara na maslahi bora ya wafanyakazi ndiyo kilio chetu, kazi iendelee'.



Mkuu wa Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma, Aziza Mangosongo kulia mwenye miwani akizindua moja ya nyumba za walimu wa Sekondari ya Kigonsera ambazo zimejengwa kwa fedha za kushirikiana na wazazi na wadau mbalimbali wa elimu .**PICHA: AMON MTEGA.**

# 'Wadau wa habari wana fursa kutoa maoni upungufu uhuru wa habari'

**Na Idda Mushi, ARUSHA**

MKURUGENZI wa Idara ya Habari (MAELEZO), Gerson Msigwa, amesema wadau wa habari bado wana fursa ya kupeleka hoja zao na maoni serikalini kuhusu maeneo wanayodhani yana upungufu wa kuminya uhuru wa habari ili wajadiliane na kuyafanyia kazi.

Msigwa alisema hayo jijini Arusha kwenye warsha ya maandalizi ya kuelekea Siku ya Uhuru wa Vyombo Habari Duniani (WPFD), inayofanyika kila mwaka, Mei 3, ambayo mwaka huu kitaifa yanafanyika jijini hapa na Rais Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi.

Alisema serikali ni sikivu na itaendelea kuimarisha uhuru wa habari kwa kuhakikisha sheria zinazotajwa kuminya uhuru wa vyombo vya habari zinaboreshwa.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Habari Kusini mwa Afrika, tawi la Tanzania (MISA-Tan), Salome Kitomari, alisema nchi kadhaa zimekuwa zikitunga sheria zinazofanana na wakati wa uchaguzi matumizi ya mitandao yamekuwa yakidhibitiwa katika nchi kadhaa jambo ambalo sio sawa.

"Ipo haja ya kuendelea kuboreshwa sheria mbalimbali za habari sio Tanzania pekee bali nchi kadhaa za kiafrika, bado kuna tatizo," alisema Kitomari.

Alisema maadhimisho hayo yanafanyika huku Tanzania ikikabiliwa na changamoto kadhaa ikiwamo ya maslahi duni ya waandishi na kwamba ipo haja ya kuwa na mipango ya muda mfupi na mrefu kukabiliana na changamoto hiyo.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, alisema mazingira ya vyombo vya habari na wanahabari kufanya kazi nchini yanaendelea kuboreshwa tofauti na miaka michache iliyopita na kwamba tayari wameanza majadiliano na serikali ya maboresho ya sheria kadhaa ambazo zinaminya uhuru wa habari.

Naye Mkurugenzi wa Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC), Dk. Ayoub Rioba, alisema tangu kuanza maadhimisho ya uhuru wa habari duniani yapo mafanikio makubwa yaliyojitokeza.

Maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa vyombo vya habari duniani yanahudhuriwa na wanahabari na wahariri wa habari kutoka mataifa mbalimbali barani Afrika na mwaka huu kaulimbiu ni 'Vyombo vya habari na changamoto za kidijitali'.

# TUCTA yalalamika wastaafu kucheleweshewa mafao

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SHIRIKISHO la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) mkoani Shinyanga, limelalamikia tatizo la wastaafu kucheleweshewa mafao.

Limesema kumekuwa na tatizo la muda mrefu kwa wastaafu kucheleweshewa mafao yao, kutoka kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii, na baadhi yao hupoteza maisha bila ya kupata.

Mratibu wa TUCTA mkoani Shinyanga, Lazaro Mnjeja, alibainisha hayo jana wakati akisoma risala kwenye maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Mei Mosi, mkoani Shinyanga, yaliyofanyika kimkoa Mjini Shinyanga katika uwanja wa michezo CCM Kambarage.

Alisema baadhi ya changamoto zinazowakabili wastaafu mkoani Shinyanga ni kucheleweshewa mafao yao, na kusababisha kukabiliwa na ugumu wa maisha.

"Mgeni rasmi ucheleweshwaji wa mafao ya kustaafu kwa wafanyakazi kutoka katika mifuko ya hifadhi ya jamii, umeendelea kuwa tatizo kubwa na wastaafu wengi na wamekuwa wakipoteza maisha hata kabla hawajalipwa mafao ya kustaafu," alisema Mnjeja.

Alitaja baadhi ya changamoto zinazowakabili wafanyakazi mkoani humo na kuhitaji zifanyiwe kazi, kuwa ni baadhi ya waajiri wa sekta binafsi hawatoi mikataba ya ajira kwa wafanyakazi na kutopeleka michango kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii.

Alitaja changamoto zingine kuwa waajiri wa sekta binafsi hawatoi hati za malipo ya mishahara, kutopandishwa madaraja, na baadhi ya waajiri kuzuia wafanyakazi wao kutojiunga na vyama vya wafanyakazi ili kutopata fursa ya kutetea maslahi yao na kuendelea kuwanyonya.

Katika hatua nyingine waliiomba serikali kulifanyia kazi suala la upandaji wa bei za bidhaa hapa nchini, ambalo limesababisha kupanda kwa gharama za maisha, na kuiomba Serikali kupandisha mishahara ya watumishi wa umma ili wamudu upandaji wa gharama hizo za maisha.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, alisema suala ucheleweshwaji wa mafao kwa wastaafu linafanyiwa kazi, na sasa hutolewa ndani ya miezi miwili na mifumo ikikaa vizuri mafao hayo yatakuwa yakitolewa ndani ya mwezi mmoja.

Alisema kwa upande wa malalamiko ya waajiri kutoka sekta binafsi, amemuagiza Katibu Tawala wa mkoa huo, Zuwena Omary, kuyafanyia kazi ndani ya mwezi mmoja, na yale ambayo ni ya kitaifa watawasilisha sehemu husika.




Watumishi wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) katika shamrashamra za Sikukuu ya Wafanyakazi Duniani, Mkoa wa Dar es Salaam, zilifanyika Uwanja wa Uhuru. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Aliyetuhumiwa kumuua mke akutwa amejinyonga

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKAZI wa kitongoji cha Tuwemacho, kijiji cha Magazini wilayani Namtumbo, Joshua Mlale (28), aliyedaiwa kumuua kwa kumkata na kisu shingoni mke wake na kumsababishia kifo kisha kukimbia, juzi amekutwa porini akiwa amefariki kwa kujinyonga.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, baadhi ya wakazi wa Kijiji cha Magazini, wamesema kuwa tukio hilo lilitokea Aprili 28, mwaka huu, baada ya kijana mmoja ambaye hawakutaka kumtaja jina akiwa anatoka shuleni kuelekea nyumbani maeneo ya porini, alikwenda kujisaidia na kumuona mtu akining'inia kwenye mti.

Wakazi hao, Selemani Ali na Rashidi Komba, walisema kijana huyo alikwenda nyumbani kwao na kuwajulisha ndugu na jamaa kuhusu tukio hilo.

Walisema baada ya taarifa hizo, watu walikimbia na kuelekea kwenye eneo hilo na kugundua anayening'inia kwenye mti ni Mlale anayetuhumiwa kumuua mke wake kwa kumchoma na kisu shingoni kisha kukimbia.

Walisema walitoa taarifa kwa uongozi wa serikali ya kijiji na kituo cha polisi.

Askari Polisi wakiwa wameongozana na daktari walifika kwenye eneo la tukio na kugundua kuwa Oshua Mlale (28), ambaye alituhumiwa kumuua mke wake kwa kumchoma kisu shingoni amefariki dunia kwa kijinyonga hadi kufa.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Joseph Konyo, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo.

Alisema Mlale alikutwa akiwa amefariki baada ya kujinyonga.

Kamanda alisema inadaiwa kuwa Aprili 25, mwaka huu, majira ya saa nne asubuhi katika kitongoji cha Tuwemacho, Amina Chande (22), aliuawa kikatili kwa kukatwa shingoni kwa kisu na mzazi mwenzake.

Kamanda Konyo alifafanua kuwa siku ya tukio baada ya kumfanyia kitendo hicho cha kinyama mke wake kutokana na mgogoro wa ndoa wa muda mrefu, alikimbia kusiko kujulikana. Polisi walikuwa wanaendelea kumsaka mpaka juzi alipokutwa akiwa amefariki dunia kwa kujinyonga.

Alisema taarifa ya awali inadai kuwa wawili hao walikuwa na mgogoro na walitengana baada ya Amina kurudi nyumbani kwao ambako sio mbali na anapoishi mume wake na Aprili 25, majira ya saa nne asubuhi, Mlale alimhadaa Amina ampe mtoto akae naye kwa muda.

Kamanda Konyo alisema, inadaiwa kuwa baadaye, Mlale alimwambia Amina aende akamchukue mtoto na alipokwenda nyumbaani kwa mume wake na kuingia nyumbani, Mlale alimkamata na kuanza kumpiga kisha kumchoma shingoni kwa kisu na kukimbia.

# Halotel kuboresha mtandao kuongeza kasi

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha wateja wanapata uhakika wa kutumia huduma za mawasiliano, Kampuni ya Halotel Tanzania imeahidi kuwekeza zaidi katika kuboresha ubora wa miundombinu ya mtandao ili kuongeza kasi ya 4G.

Mkurugenzi wa Kituo cha Biashara cha Halotel, Abdallah Salum, alisema kuwa kampuni hiyo katika maeneo yote ilipo nchini imeongeza wigo wa mtandao takribani nchi nzima na kufikia asilimia 95 ya Watanzania.

"Katika miaka miwili ijayo, tutawekeza zaidi kwenye miundombinu ili kuhakikisha huduma bora za mawasiliano ili kuongeza ubora wa huduma," alisema, na kufafanua kuwa kuna mipango mingine kama kupanua wigo na lengo ni kuwekeza zaidi kwenye kizazi cha nne mtandao ili kukidhi mahitaji yanayoongezeka kutoka kwa Watanzania.

"Kampuni inaendelea kutandaza minara ya 4G katika maeneo mbalimbali nchini, ambapo huduma hizo hazijawahi kuwapo hapo awali. Lengo ni kuwa na wateja wengi walioboresha nambari yao ya 3G hadi 4G," alisema.

"Tunasaidia wateja wetu kutumia huduma ya mtandao ya kasi ambayo ni rahisi sana kulingana na mahitaji yao."

Halotel, kampuni tanzu ya Viettel International ya Vietnam imepewa kandarasi na serikali kupanua miundombinu ya mawasiliano hadi maeneo ya vijijini ambapo kampuni zinazoongoza za mawasiliano ya simu zilishindwa kuwekeza kwa sababu ya soko duni.

Alisema kampuni za mawasiliano zilizopewa kandarasi na serikali kusambaza huduma za mawasiliano katika maeneo ya vijijini yaliyotengwa mwaka 2015, zinalenga kuongeza watumiaji wake kutoka milioni saba hadi milioni 10 ifikapo 2023.

Kwa muujibu wa Salum, hadi kufikia sasa, wamesambaza minara 800 ya mawasiliano ya kizazi cha nne katika kipindi cha miaka sita ili kueneza mawasiliano ya kidijitali kote nchini.

Alisema kuwa minara ya 4G pia imesambazwa katika mikoa yote ya Zanzibar huku sehemu kubwa ikiwa katika maeneo ya mbali.

"Kama Halotel tumefurahi sana kwa utendaji kazi huu, tutaendelea kuboresha kasi ya mtandao wetu ili kuwaruhusu wateja wetu kufurahia huduma za intaneti katika maeneo yote walipo na huduma nyinginezo," alisema.

# WCF yapata tuzo tatu za usalama, afya mahali pa kazi

**Mwandishi Wetu,** DODOMA

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umepata tuzo tatu katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi Duniani.

Akizungumza wakati wa kilele hicho, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Prof Joyce Ndalichako amewataka waajiri na wafanyakazi kuendelea kushirikiana pamoja ili kuweka mazingira yenye usalama na afya katika maeneo ya kazi ikiwemo kuzuia vihatarishi.

Amefafanua kuwa, kuweka mazingira salama kunapunguza gharama kwa sababu wafanyakazi wanapopata ajali au ugonjwa kutokana na kazi inavuruga mipango ya uzalishaji kwa pande zote mbili.

"Waajiri na wafanyakazi ni lazima wafahamu suala la afya na usalama mahali pa kazi ni mkakati wa pamoja na ni sehemu ya utekelezaji wa Mfumo wa haki na wajibu ulioainishwa kimataifa na kanuni ya kuzuia vihatarishi inapewa kipaumbele cha juu zaidi,", alieleza Ndalichako.

Wakati huohuo, Shirika la Kazi Duniani (ILO) limeahidi kushirikiana na Serikali ya Tanzania kupitia WCF kushughulikia masuala ya fidia kwa wafanyakazi wanaoumia, kuugua au kufariki kutokana na kazi.

Ahadi hiyo ilitolewa na Mwakilishi wa Shirika hilo, Getrude Sima, baada ya WCF kushinda tuzo tatu katika maadhimisho ya Siku ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi Duniani ambapo kwa Tanzania yamefanyika jijini Dodoma.

"Tutaendelea kushirikiana na WCF kupitia mikakati yetu mbalimbali ndani ya Shirika la Kazi Duniani hapa Tanzania kwa hiyo niwapongeze sana na nimefurahi kuona kwamba nanyi pia mmeweza kushiriki na kuwaeleza wananchi mnachofanya," alisema Sima.

Naye Katibu Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), Hery Mkunda, aliipongeza WCF kwa kushinda tuzo nyingi zaidi na kuitaka taasisi hiyo kuendelea kuwa mfano wa kuigwa barani Afrika.

Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dk. John Mduma, alisema mfuko huo umeshalipa fidia kwa wafanyakazi mbalimbali waliopata ajali wakiwa kazini na baadhi yao walishiriki katika maadhimisho hayo.

Kuhusu huduma zilizotolewa alisema WCF imeshirikisha wanufaika wao katika kutoa elimu ya fidia kwa wadau waliotembelea maadhimisho hayo. Pia imeweza kuonyesha viungo bandia vinavyolipiwa na WCF kwa wahitaji wa viungo hivyo, pamoja na uwepo wa madaktari tunaoshirikiana nao katika utoaji wa huduma mbalimbali za kitabibu", amehabarisha Dkt Omar.

Wanufaika wa mfuko huo, waliishukuru serikali kwa kuanzisha WCF ambayo imeweza kuwalipia gharama za matibabu, kuwanunulia viungo bandia ikiwemo miguu na mikono bandia pamoja na kuwalipa pensheni kila mwezi huduma ambayo itaendelea mpaka mwisho wa uhai wao.

HABARI KITAIFA

# GGML yaibuka kinara usalama mahala pa kazi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Geita Gold Mining Limited (GGML) imeibuka mshindi wa jumla katika maonesho ya afya na usalama mahala pa kazi yaliyofanyika jijini Dodoma.

Maonesho hayo ya afya na usalama mahala pa kazi yameratibiwa na Wakala wa Afya na Usalama Mahala pa Kazi nchini (OSHA) katika kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Afya na Usalama Mahala pa Kazi ambayo huadhimishwa duniani Aprili 28 kila mwaka.

Pia OSHA imeipatia GGML tuzo ya kampuni bora inayoifikia zaidi jamii katika uelimishaji wa masuala ya afya na usalama kwenye maeneo yao.

Akizungumza katika hafla ya kuadhimisha siku ya Kimataifa ya Afya na Usalama Mahala pa Kazi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, aliipongeza kampuni ya GGML kwa kutoa kipaumbele kwenye afya na usalama wa wafanyakazi na kutoa wito kwa kampuni nyingine nchini kuwekeza katika kuboresha mazingira ya afya na usalama wa wafanyakazi wao.

"Waajiri wengi nchini hawatoi msisitizo kwenye masuala ya afya na usalama kwa sababu ya kuogopa gharama. Lakini linapokuja suala la ajali na vifo, gharama huwa ni kubwa zaidi na kuwaathiri waajiri wenyewe, kampuni, wafanyakazi, jamii, taifa na uchumi kwa ujumla.

"Tuendelee kushirikiana kujenga utamaduni bora wa afya na usalama mahala pa kazi kama kauli mbiu ya siku ya afya na usalama mahala pa kazi mwaka huu inavyosema," aliongeza Prof. Ndalichako.

Meneja Mwandamizi wa GGML anayeshughulikia masuala ya afya, usalama, mazingira na mafunzo, Dk. Kiva Mvungi, alisema siri ya kampuni ya GGML kuibuka kidedea katika masuala ya afya na usalama kwa muda mrefu ni kuwa na utamaduni bora wa kushirikisha wafanyakazi na makandarasi wake na ndiyo maana imeweka suala la usalama kuwa kipaumbele chake cha kwanza katika shughuli zake.

"Changamoto ya ajali na vifo mahala pa kazi ni suala linaloathiri wafanyakazi wengi duniani pamoja na familia zao. Tumejitahidi kuzuia vifo na ajali katika mgodi wetu ndiyo sababu hatujapata ajali ya kuondoa maisha ya mfanyakazi ndani ya mgodi kwa zaidi ya miaka 10 hivi sasa.

"Mara ya mwisho mtu kupata majeraha yaliyomzuia kuendelea na kazi ilikuwa mwaka 2018 wakati mwaka 2017 tulipata tukio moja la mtu kupata jeraha dogo lilomzuia kuendelea na kazi.

"Hii kwetu ni rekodi nzuri ukilinganisha na migodi mingine na tunaendelea kuwaelimisha wafanyakazi wetu kuendelea kuwa makini na kufuata taratibu zote za usalama wanapokuwa kazini ili tuhakikishe tunaendelea na rekodi yetu ya kuwa mgodi kinara katika kuzingatia usalama kuliko migodi yote duniani,"alisema Dk. Mvungi.

Alisema miongoni mwa kampuni zote za AngloGold Ashanti ambayo ni kampuni mama ya GGML imeendelea kuwa kampuni bora ya kwanza inayozingatia usalama kwa kiwango kikubwa.

Ameongeza kuwa kampuni ya GGML inathamini maisha ya wafanyakazi na makandarasi wake na ndiyo maana imeweka suala la usalama kuwa kipaumbele chake cha kwanza katika shughuli zake.

"Tumekuwa tukishirikiana na OSHA kila mwaka kuielimisha jamii na taasisi zinazoshiriki katika maonesho haya mifumo na teknolojia za kuboresha afya na usalama sehemu zetu za kazi.

"Lengo ni kuikumbusha jamii kuwa maisha na uhai ni jambo la msingi kuliko hata uchumi au faida ambayo inaweza kuzalishwa na kampuni," alisema Dk Mvungi.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako akimkabidhi Meneja Mwandamizi wa GGML anayeshughulikia masuala ya afya, usalama, mazingira na mafunzo Dk. Kiva Mvungi tuzo. Kulia kwake ni Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri kutoka OSHA, Dk. Adelhelm James Meru. GGML imeibuka mshindi wa jumla katika maonyesho ya usalama na afya mahala pa kazi jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampeni chanjo UVIKO-19 kufanyika mtaa kwa mtaa

**Na Sabato Kasika**

HALMASHAURI ya Wilaya Morogoro inatarajia kuanza kampeni maalum ya mtaa kwa mtaa kwa ajili ya kuhamasisha chanjo ya UVIKO-19 ambayo itahusisha viongozi kuanzia ngazi ya kitongoji hadi wilaya. Kampeni hiyo ya mwezi mmoja, itaanza Mei mosi mwaka huu, huku wanaotarajiwa kuhusika ni watoa chanjo, viongozi kutoka ngazi ya vitongoji, vijiji, madiwani, watendaji wa kata na mkuu wa wilaya.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, Lucas Lemomo, alipokuwa akizungumza na gazeti hili jana na kufafanua kuwa hiyo itakuwa ni awamu ya pili ya kampeni zao.

"Kwenye suala la chanjo tuko vizuri, tulishawahi kuwa na kampeni kwa kila diwani kuhamasisha katika kata yake, sasa tunakuja na kampeni ya pamoja kuanzia viongozi wa vitongoji hadi wilaya," alisema Lemomo.

Alisema, wanajiandaa kuja na kampeni ya mtaa kwa mtaa kwa kuwa anaamini kwamba suala la chanjo linahitaji hamasa kutokana na imani ambayo imejengwa miongoni mwa jamii ya kutoamini chanjo.

"Tunaamini kampeni hii ambayo itaanza Mei mosi itasaidia kubadilisha mtazamo wa watu wengi ambao awali walikuwa hawataki kuchanja na kuegemea kwenye nyungu wakihofia usalama wa chanjo," alisema.

Alisema, yeye na madiwani wote walishachanjwa, na kwamba watahamasisha wakiwa na uhakika wa huduma hiyo, huku wakisaidiana na watoa chanjo ambao wataelimisha umma kuhusu umuhimu wa kuchanja.

Alifafanua kuwa kampeni hiyo itakwenda sambamba na uhimizaji wa kufuata mwongozo wa Wizara ya Afya unaotaka kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima kunawa mikono kwa maji tiririka na kutumia vitakasa mikono. "Tunataka kampeni hii ya kumahasisha chanjo iende sambamba na uzingatiaji wa mwongozo huo kwa ajili ya usalama zaidi, hivyo ninaomba wote tuungane kuanzia Mei mosi kufanikisha jambo hili muhimu, lakini pia tutahamasisha chanjo ya polio," alisema.

Diwani wa Kata ya Gwata, Zongo Lobe Zongo, alisema kwenye suala la chanjo la UVIKO-19, chini ya mwenyekiti wao wa halmashauri wamekuwa wakibuni mbinu mbalimbali za kuhakikisha wananchi wanapata huduma hiyo.

# Prof Ngowi: Jinsi ya kujiajiri kihalali

**Na Jenifer Gilla**

MWANZONI mwa mwaka huu kabla ya umauti haujamkuta aliyekuwa Profesa wa Uchumi katika Chuo Kikuu cha Mzumbe, marehemu Prof. Honest Ngowi, alialikwa katika hafla ya kiroho naye akabarikiwa kutoa somo la jinsi ya kujiongezea kipato kihalali.

Prof. Ngowi alifungua somo hilo kwa kusema kuwa siku zote vipato havijitoshelezi kwa kuwa kadiri maisha yanavyosonga ndivyo mahitaji yanaongezeka hivyo hata kama kipato chako ni kikubwa kuna haja ya kufanya juhudi za kukiongeza bila kuvunja sheria ya nchi na kwenda kinyume na matakwa ya Mungu.

Alisema lengo la kujiongezea kipato ni kumwezesha mjasiriamali kumudu kugharamia mahitaji ya msingi kama vile elimu, malazi na chakula.

Alisema moja ya njia ya kujiongezea kipato ni kutumia fursa zinazokuzunguka kufanya biashara akitolea mfano wa wajasiriamali waliojitokeza mahali hapo kuuza bidhaa zao kwa kuwa tu siku hiyo kulikuwa na warsha ambayo ilijumuisha watu wengi.

"Kabla sijaingia hapa nilifanya 'study' kidogo, nikazunguka nje huko nikaenda mpaka kule juu nikaona baadhi ya watu wametumia fursa ya umati uliokuja katika mkutano huu kwamba ni fursa na hiyo ni sahihi sana.

Kwa hiyo kama tuna shughuli za kutuingizia vipato halafu hatujatumia hii fursa ya huu umati tuliokutana hapa, tunasema ni fungu la kuchekwa,"alisema.

Alisema ujasiriamali unaweza kufanywa na mtu yoyote awe kijana au mzee, mwanamke au mwanaume, wa kutoka dhehebu lolote ili mradi tu biashara hiyo inafanyika kwa njia ya halali.

Mchumi huyo aliongeza kuwa ili uweze kufanya ujasiriamali na kupata matokeo chanya ni lazima uwe na uthubutu wa hali ya juu kwa sababu kama ilivyo sekta nyingine na yenyewe ina changamoto zenye kukatisha tamaa.

"Ukiwa muoga hutoweza, kwa sababu tunachosema kuwa ujasiriamali kwa maana ya kusoma tungesema sio Sunday School, huendi kusoma A,B,C, ni mambo mazito.Ukiogopa kuanza hicho unachotaka kuanza kwa sababu yoyote ile huwezi kuwa mjasiriamali mzuri." Alisema.

Aliongeza kuwa ili uwe mjasiriamali au uweze kujiajiri huna budi kuwa mbunifu kwa sababu kule hakuna biashara mpya, kila biashara imeshafanyika na tayari ipo sokoni, hivyo unahitaji kuwa mbunifu ili ujitofautishe na waliokutangulia.

Alisema kingine biashara inahitaji kujitoa na kujituma usiku na mchana hivyo mjasiriamali anapoamua kuanzisha biashara atambue kuwa kuna wakati atakosa hata muda wa kupumzika na kulazimika kuchelewa kulala na kuwahi kuamka.

Alisema njia nyingine ni kufanya ujasiriamali jamii, biashara ambayo faida inayotengenezwa sio kwa maslahi binafsi bali ni ya kuendeleza kigango. Alisema huu huhusisha zaidi vyama vya kitume kama vile WAWATA.

"Kwamba tunafanya ujasiriamali sio kwa faida binafsi, kama ni WAWATA, kama ni UWAKA, kama ni wale vijana watumishi kule kanisani mmeamua kufanya shughuli zenu za ujasiriamali, kama ni parokiani faida sio binafsi, sio faida ya kuingia mfukoni, ni faida ya kuendeleza kigango, parokia, jimbo," alifafanua Prof Ngowi.

Prof alisema kuwa mchakato wa kujiajiri ni kama kujenga ROMA mbayo ilichukua miaka mingi, akimaanisha kuwa ni mchakato unaochukua muda mrefu hadi biashara kuwa imara na ndani yake kuna changamoto nyingi hivyo uvumilivu unahitajika.

# Mamalishe azoa mil. 25/- Mwaa Mwii na Tigopesa

**Na mwandishi Wetu**

Mkazi wa Kigamboni mkoani Dar es Salaam, Suzanne Daniel ameibuka mshindi wa promosheni ya Kampuni ya utoaji wa huduma za kidigitali yaTigo.

Suzanne, ambaye ni mamalishe, amejipatia Sh. milioni 25 za Tigo Tanzania ilipofunga safari ya kumfuata mshindi wa droo kubwa ya Sh. milioni 25 ya promosheni ya Pesa Mwaa Mwii na Tigopesa.

Suzzanne aliibuka mshindi Aprili 25, 2022 ambapo Droo ya fainali ilichezeshwa katika ofisi za Tigo Makao Makuu jijini Dar es Salaam. Mbali na Suzzanne walipatikana pia washindi 10 wa Sh. milioni 10 kila mmoja.

Akizungumza wakati wa kumkabidhi mshindi hundi ya Sh. milioni 25, Meneja wa Kitengo cha wateja Binafsi Tigo Pesa, Mary Rutta aliwapongeza wateja wote walioibuka washindi wa zawadi mbalimbali na pesa taslimu katika promosheni hiyo na kuwasihi wateja wengine ambao hawakubahatika kushinda kuendelea kutumia Tigo Pesa maana kuna mambo mengi na mazuri yanakuja.

" Kama ilivyo kawaida yetu Tigo Pesa hatujawahi kuishiwa kutoa zawadi na mambo mengine mazuri kwa wateja wetu. Leo tunamkabidhi mshindi wetu mkubwa wa promosheni yetu Suzzanne zawadi yake ya Sh. million 25, lakini niwasihi wateja wetu kuendelea kutumia huduma zetu maana kutumia Tigo Pesa kunalipa."

Suzanne, mamalishe (41) aliipongeza sana Tigo Tanzania kwa kuwajali wateja wake na kuamua kuwarudishia fadhila kupitia promosheni mbalimbali

" Kwakweli sikuamini baada ya kupigiwa simu na kuambiwa kwamba nimeshinda milioni 25 kutoka promosheni ya Pesa Mwaa Mwii , nilihisi kama muujiza, lakini namshukuru Mungu leo nakabidhiwa Sh. milioni 25 ambazo zitanisaidia kuongeza biashara yangu ya uuzaji wa chakula , Mungu awabariki sana Tigo hakika nimeamini kutumia Tigo Pesa kunalipa nawasihi watanzania wasizipuuze promosheni mbalimbali zinazotangazwa na Tigo huenda wakawa wenye bahati na wakabadilishiwa maisha yao kama ambavyo leo Tigo wanaenda kubadilisha maisha yangu." alisema. Walioibuka washindi kwenye promosheni hii ni waliofanya miamala mara nyingi kupitia huduma za Tigo Pesa ikiwa ni pamoja na lipa kwa simu, malipo ya bili, malipo ya serikali, miamala ya mtandaoni kutoka kwa wenzao na kupokea pesa kutoka kwa mtandao mwingine wa simu.

# Zaidi ya nyumba 500 Pwani zimeingizwa anwani za makazi

**Na Julieth Mkireri,** RUFIJI

HADI kufikia Aprili 29, mwaka huu nyumba za makazi 515,668 zimeingizwa kwenye mfumo wa anwani za makazi mkoani Pwani.

Hayo yamebainishwa na Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge jana wilayani Rufiji alipokuwa akipokea Mwenge wa Uhuru kutoka mkoani Lindi.

Alisema kwa sasa zoezi la anwani za makazi katika mkoa huo limefikia asilimia 105.61.

Alisema mkoa huo umepokea Sh. milioni 816.2 kutoka Serikali Kuu na kwa upande wa halmashauri zimechangia Sh. milioni 320 kutekeleza anwani za makazi kwa mkoa huo.

Akizungumzia upande wa miradi itakayotembelewa na Mwenge, Kunenge alisema miradi 111 yenye thamani ya Sh. bilioni 69 .2 itatatembelewa, kati ya hiyo 25 itawekewa mawe ya msingi, 22 itazinduliwa, sita itafunguliwa na 58 itakaguliwa.

Kiongozi wa mbio za Mwenge kitaifa, Sahil Geraruma, alitoa maelekezo kwa Mkoa wa Lindi kuzingatia maagizo yaliyotolewa kwenye miradi ya maendeleo iliyokaguliwa.

Vile vile, alisema Mwenge wa Uhuru hautaondoka kwenye halmashauri ambazo fedha za mfuko wa maendeleo ya vijana zilikopeshwa na hadi sasa hazijarejeshwa sehemu husika.

"Fedha hizo zilikopeshwa kwa vijana wakazirejesha kwa wakati eneo husika, lakini cha kusikitisha halmashauri hizo hazijazirejesha fedha hizo katika mfuko wa vijana ofisi ya Waziri Mkuu," alisema.

Alisema jambo hilo ni la kusikitisha ambalo limesababisha kudhoofisha mfuko wa vijana na kurudisha nyuma maendeleo yao na kwamba halmashauri zote nchini wanatakiwa warejeshe fedha hizo za vijana kwa wakati.

Akipokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Meja Edward Gowele, alisema utakimbizwa katika miradi sita yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 6.5.




Wafanyakazi wa Benki ya NMB wakipita mbele ya Rais Samia Suluhu na bango lao wakati wa kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani, iliyofanyika kitaifa jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Machinga watakiwa kuthibitisha ubora wa bidhaa

**Na Mwandishi Wetu**

WAMACHINGA wametakiwa kujitokeza Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kwa ajili ya kuthibitisha ubora wa bidhaa zao ili waweze kufikia viwango vya ushindani katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Ofisa Usalama wa Chakula Mwandamizi wa TBS, Imakulata Justin wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Biashara kwa wafanyabishara Wadogo yajulikanayo kama Machinga Complex Day yaliyofanyika jijini Dar es Salaam kuanzia Aprili 25 hadi 30,mwaka huu.

Alisema wao kama Shirika wameshiriki maonyesho hayo kwa lengo la kutekeleza majukumu yao, ikiwemo la utoaji elimu kwa wazalishaji kuhakikisha wanakidhi matakwa ya viwango.

Alisema kwa kuthibitisha bidhaa wanazozalisha kuna faida mbalimbali, mojawapo kama wazalishaji inawapa uwezo mkubwa wa kushindana kwenye soko, kwani bidhaa inapokuwa imethibitishwa ubora inakuwa na ushindani mkubwa hivyo itapata wateja wengi.

Faida nyingine ya kuthibitisha ubora wa bidhaa kwa mujibu wa Justin ni kumuondolea usumbufu mzalishaji, kwani bidhaa hiyo haitakiwi kupimwa mara kwa mara ili kuweza kukidhi matakwa ya mnunuzi.

"Mnunuzi anapokuja kufanya manunuzi kama bidhaa yako haijathibitishwa ubora wake, basi utalazimika kuipima mara kwa mara ili mnunuzi aweze kuridhika na kununua bidhaa hiyo.

Kwa hiyo huo ni usumbufu na ili kuondoa huo usumbufu ukithibitisha ubora yako basi inakuwa inaaminika na inakuwa ni kinga dhidi ya ushindani wa bidhaa duni zisizo na ubora, kwani zenyewe zitakuwa hazipati soko zuri," alisema Justin.

Aidha, alisema kwa mlaji hiyo inamthibitishia kuwa bidhaa husika inafaa kwa matumizi yaliyokusudiwa, hivyo akiiona anakuwa na imani na inamwezesha kukua kwa bei katika soko na kuwahakikishia usalama wateja wake kiafya.

Justin alisema ili kuthibitisha bidhaa za wajasiriamali wadogo, TBS ina mpango maalum wa kuwasaidia kuthibitisha bidhaa zao bure, kwani gharama zao zinalipwa na Serikali

Alifafanua kwamba wanachotakiwa kuwa nacho ni barua ya utambulisho kutoka SIDO na kwamba wakifika nayo TBS, Shirika linaanza mchakato wa kuwathibitishia bidhaa zao.

"Kwa hiyo mzalishaji anapokuwa na barua ya utambulisho anaweza kuingia kwenye mfumbo wa TBS ambao unapatika kwenye tovuti ya shirika na kwenda kwenye eneo husika kwa ajili ya kuomba idhini ya kutumia alama ya ubora," alisema na kuongeza:

"Mjasiriamali atatakiwa kujaza taarifa zake katika mfumo akiambatanisha na viambatanisho vinavyotakiwa ikiwemo leseni ya biashara , utambulisho wa mlipa kodi na barua ya utambulisho kutoka SIDO.

Maombi yakishafika kwenye shirika yanafanyiwa kazi na mjasiriamali atafahamishwa kuwa wakaguzi wa TBS wataenda kwake kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa awali."

NIPASHE JUMATATU MEI 2, 2022

Nipashe

Spotika




WACHEZAJI 10 WALIOFUNGA HAT-TRICK EPL MSIMU HUU UK. 12-13



# MAMBO MATANO USIYOYAJUA KUHUSU TEN HAG WA UTD

## ISIKUPITE

KATIKA historia ya Ligi Kuu England, Ole Gunnar Solskjaer ndiye mchezaji anayeshikilia rekodi ya kufunga mabao mengi (4) zaidi kwenye mechi moja akitokea benchi. Solskjaer alifunga mabao manne Manchester United ikishinda 8-1 dhidi ya Nottingham Forest msimu wa 1998/99, alipotokea benchi dakika ya 72 wakati huo United ikiwa mbele kwa mabao 4-1, bao lake la kwanza lilikuja dakika ya 80, la pili dakika ya 88 na kukamilisha 'hat-trick' dakika chache baadaye kabla ya dakika za majeruhi kutupia la nne.



**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United imetangaza kumteua, Erik ten Hag kuwa kocha wao mpya wa kudumu msimu ujao. Kocha huyo mkuu wa sasa wa Ajax, ataanza kazi pale Old Trafford baada ya kumalizika kwa msimu huu.

Mholanzi huyo atakuwa kocha wa tano wa Man United katika muongo mmoja baada ya Sir Alex Ferguson kustaafu mwaka 2013. Kazi kubwa ya Hag ni kubadilisha hali ya soka pale Old Trafford.

Jukumu lake la kwanza kama kocha mkuu lilikuja mwaka 2012 akiwa na klabu ya Uholanzi ya Go Ahead Eagles. Hiyo ilifuatiwa na miaka miwili katika timu ya akiba ya Bayern Munich na miaka mitatu kule Utrecht ya Uholanzi.

Mholanzi huyo mwenye umri wa miaka 52, kwa sasa anainoa Ajax ambayo alijiunga nayo mwaka 2017. Ten Hag ameiwezesha klabu hiyo kutwaa mataji mawili ya ligi, mataji mawili ya KNVB na mataji mawili ya Ngao ya Johan Cryuff. Timu yake ya Ajax ilikuwa kileleni mwa ligi kabla ya msimu wa Ligi Kuu Uholanzi wa 2019-20 kufutwa kwa sababu ya janga la COVID-19.

Kwa sasa wako mbele kwa pointi nne juu msimamo wa ligi huku wakiwa wamebakiwa na mechi tano za ligi na wanapewa nafasi kubwa ya kutwaa ubingwa wa msimu huu wa 2021-22. Ajax pia walifika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2018-19 chini ya Ten Hag.

Hapa tunaangalia mambo matano ya kuvutia kuhusu bosi huyu wa Man United, twende sasa.

### #5. Ni kocha wa haraka zaidi kufikisha ushindi mara 100 akiwa na Ajax

Ajax wana historia nzuri na wamefundishwa na baadhi ya watu wenye akili kubwa katika historia ya mchezo huo. Johan Cryuff, Rinus Michels, Louis van Gaal, Jack Reynolds na Leo Beenhakker ni baadhi ya wachezaji wenye majina makubwa waliotamba na klabu hiyo ya Uholanzi.

Hakuna kocha mwingine aliyewahi kufikisha ushindi wa mechi 100 kwenye Ligi Kuu ya Uholanzi, Eredivisie, akiwa na klabu hiyo. Alihitaji mechi 128 ili kupata ushindi mara 100 akiwa na klabu, hivyo kuweka rekodi mpya. Cha kufurahisha ni kwamba, aliyekuwa anashikilia rekodi hiyo alikuwa bosi wa zamani wa Manchester United, Louis van Gaal, ambaye alifanya hivyo katika mechi 137.

### #4. Alikuwa mlinzi wakati wa uchezaji wake

Kabla ya kuingia katika ulimwengu wa ukocha, Hag alifurahia uchezaji wa kawaida uliodumu kutoka mwaka 1989 hadi 2002. Mholanzi huyo alikuwa akicheza nafasi ya beki wa kati.

Aliichezea Utrecht michezo 31 na akajipatia jina akiwa FC Twente, akicheza michezo 248. Ten Hag hakuwahi kuichezea timu ya taifa na alishinda kombe moja katika maisha yake - Kombe la KNVB la 2002 akiwa na Twente.

### #3. Anapenda kucheza dansi

Akiwa mtoto, Erik ten Hag aliripotiwa kujihusisha na soka na kucheza. Alilelewa katika mji wa Haaksbergen, ulio katika eneo la Twente mashariki mwa Uholanzi.

Ingawa kipaji chake cha kucheza mpira wa miguu kilionekana tangu utoto, Mholanzi huyo pia alikuwa dansa mwenye shauku na alihudhuria madarasa kadhaa ya kudansi.

### #2. Timu alizofundisha hazijawahi kumaliza chini ya sita bora

Timu kumi za Hag zimefanya vema kwenye mashindano ya ligi katika kipindi cha maisha yake ya ukocha. Mwisho wa chini kabisa wa ligi katika taaluma yake ya usimamizi ulikuja na Go Ahead Eagles katika msimu wake wa kwanza kama kocha mkuu; walimaliza nafasi ya sita kabla ya kupandishwa daraja hadi Eredivisie.

Kwa upande wa ligi ya juu, mwisho wa chini kabisa wa Ten Hag kwenye Eredivisie ulikuja na Utrecht msimu wa 2015-16. Walimaliza nafasi ya tano katika mwaka wake wa kwanza na klabu hiyo.

### 1#. Alifanya kazi na Guardiola kule Bayern

Hag alikaa Ujerumani kwa miaka miwili alipokuwa akisimamia timu ya akiba ya Bayern Munich, akishinda michezo 48 kati ya 72 aliyoiongoza. Wakati huo, alipata fursa ya kufanya kazi na Pep Guardiola, ambaye sasa ni kocha mkuu wa Manchester City.

Mhispania huyo anatambulika sana kama mmoja wa makocha wenye ushawishi mkubwa katika mchezo huo. Mfumo wa kushambulia na kumiliki mpira wa Guardiola umewatia moyo makocha wengi akiwamo Ten Hag. Februari 2019, Mholanzi huyo alisema:

"Nilijifunza mengi kutoka kwa Guardiola. Falsafa yake ni ya kusisimua; alichokifanya Barcelona, Bayern na sasa akiwa na Manchester City, mtindo huo wa kushambulia na kuvutia unamuona akishinda sana. Ni muundo huu ambao nimejaribu kuutekeleza nikiwa na Ajax."

Mtazamo wa falsafa ya Guardiola unaonekana pale Ajax ya Ten Hag, ambayo inacheza soka ya kasi na ya kuvutia.

## Extra Time

# WACHEZAJI 10 WALIOFUNGA HAT-TRICK EPL MSIMU HUU

**LONDON,** England

KABLA ya mechi za wiki iliyopita, jumla ya mabao 895 yamefungwa kwenye Ligi Kuu England (EPL). Mabao 33 kati ya hayo yamepatikana kama hat-trick kutoka kwa wachezaji 10 tofauti.

**Kufunga bao kwenye Ligi Kuu England ni kazi ngumu, kwa hiyo kutupia mabao matatu katika mchezo mmoja si jambo rahisi. Nyota wa zamani wa Manchester City, Sergio Aguero anashikilia rekodi ya kufunga hat-trick nyingi kwenye Ligi Kuu (12).**

Mwanasoka anapofunga hat-trick, anarudi nyumbani na mpira wa siku ya mechi. Makala haya inawaangalia wachezaji 10 waliofunga hat-trick msimu huu wa Ligi Kuu, haya sasa...

### #1. Bruno Fernandes

Nyota wa Manchester United, Bruno Fernandes ndiye mchezaji wa kwanza kufunga mabao matatu katika mchezo mmoja msimu huu kwenye Ligi Kuu England. Mreno huyo alifunga bao lake la kwanza kabisa la Ligi Kuu siku ya kwanza ya mechi. Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa hat-trick kufungwa katika mechi ya siku ya ufunguzi wa msimu huu.

Fernandes alikamilisha hat-trick yake katika muda wa dakika 30 katika vipindi vyote viwili Manchester United ilipoichabanga Leeds United 5-1 kwenye uwanja wa Old Trafford. Amefunga mabao sita zaidi, na kufikisha jumla ya mabao tisa katika Ligi Kuu England katika mechi 31 alizocheza.

### #2. Roberto Firmino

Claudio Ranieri alipokea kichapo kikubwa katika mechi yake ya kwanza kama kocha wa Watford na Roberto Firmino ndio aliyewaua. Mshambuliajihuyo wa Brazil alifunga mabao matatu wakati Liverpool ilipoilaza Watford 5-0 kwenye Uwanja wa Vicarage Road Oktoba 16, 2021.

Majeraha ya mara kwa mara yamemfanya Firmino kuwa nje ya uwanja, lakini bado ameweza kufunga mabao matano katika mechi 18 za ligi msimu huu.

### #3. Mason Mount

Mason Mount ndiye mchezaji pekee wa Chelsea aliyefunga hat-trick msimu huu. 'Mchezaji Bora wa Mwaka' wa Chelsea alifunga bao lake la tatu katika maisha yake ya soka Stamford Bridge katika ushindi wa Chelsea wa mabao 7-0 dhidi ya Norwich waliokuwa kwenye hatari ya kushuka daraja.

Mount aliwafungia 'Blues' bao la kwanza, la sita na la mwisho, na kuwa mchezaji wa 81 wa Chelsea kufunga hat-trick. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, hajatazama nyuma tangu wakati huo. Akiwa na mabao 10 na asisti tisa, ndiye mchangiaji bora wa mabao wa Chelsea kwenye Ligi Kuu England.

### #4. Joshua King

Kufunga bao moja dhidi ya klabu yake ya zamani kunakuja kwa hisia tofauti, lakini kwa Joshua King, kufunga mabao matatu dhidi ya klabu yake ya zamani kilikuwa kitu cha aina yake.

King alitumia msimu uliopita kule Everton, lakini hakupewa muda wa kutosha kucheza. Raia huyo wa Norway alicheza mara 11 pekee kwa 'The Toffees' hao.

### #5. Mohammed Salah

Siku chache zilizopita, Salah aliweka rekodi ya kuwa mchezaji wa kwanza kufunga mabao matano dhidi ya Manchester United ndani ya msimu mmoja. Mmisri huyo mwenye umri wa miaka 32, alifunga mabao matatu pale Old Trafford na mawili Anfield.

Kuichapa Manchester United 5-0 kwenye uwanja wao wa nyumbani ilikuwa jambo la kushangaza, kwani Salah alikuwa mchezaji wa kwanza kufunga mabao matatu dhidi ya United kwenye Ligi Kuu. Salah kwa sasa ana hat-trick nne za Ligi Kuu na anaongoza kwenye mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu akiwa na mabao 22 kwenye ligi msimu huu.

### #6. Jack Harrison

Winga wa Leeds United, Jack Harrison ndiye aliyefunga hat-trick ya sita msimu huu. Nyota huyo wa zamani wa Manchester City aliiwezesha timu hiyo ya Yorkshire kupata ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya West Ham. Pia amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga hat-trick dhidi ya timu hiyo ya London tangu mwaka 1927. Hadi sasa, Harrison amefunga mabao saba na kutoa asisti moja katika mechi 29 za ligi.

### #7. Raheem Sterling

Manchester City wana macho yao kwenye taji lingine la ligi na mchezaji mmoja ambaye amekuwa na jukumu muhimu katika mbio hizo ni Raheem Sterling. Siku ya nane ya mechi, mshambuliaji huyo wa England alifunga mabao matatu katika ushindi wa 4-0 wa City dhidi ya Norwich kwenye Uwanja wa Carrow Road.

Hiyo ilikuwa hat-trick ya tano kwa Sterling kwenye Ligi Kuu na kufikia sasa, ana mchango wa mabao 13 kwenye ligi - mabao 10 na asisti tatu.

### #8. Ivan Toney

Norwich walifungwa hat-trick nyingine, safari hii kutoka kwa Brentford iliyopanda daraja. 'Nyuki' hao walipata ushindi wa mabao 3-1 wakiwa ugenini na kujiongezea nafasi ya kukwepa kushuka daraja. Mshambuliaji, Ivan Toney alifunga mabao yote matatu na kumaliza msururu wa michezo nane bila kushinda.

Pia akawa mchezaji wa kwanza wa Brentford kufunga hat-trick kwenye Ligi Kuu. Toney amekuwa mfungaji bora wa Brentford msimu huu akiwa amefunga mabao 13 na asisti tano katika mashindano yote.

### #9. Heung-Min Son

Matumaini ya Tottenham kurejea kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya yamekuwa chanya kutokana na kocha Antonio Conte na mabao ya Heung-Min Son. Mchezaji huyo aliandikisha ushindi wake wa pili wa Ligi Kuu katika ushindi wa 4-0 dhidi ya Aston Villa wiki chache zilizopita pale kwenye Uwanja wa Villa Park.

Baada ya kutangulia kufunga kipindi cha kwanza, nyota huyo wa Korea Kusini akafunga mabao mawili kipindi cha pili, na kuamsha matumaini ya Tottenham ya kumaliza katika nne-bora. Akiwa na mabao 17 kwenye ligi, Son ndiye mfungaji bora wa Spurs na pia anawania Kiatu cha Dhahabu.

### #10. Cristiano Ronaldo

Mafanikio ambayo Cristiano Ronaldo anaendelea kufikia akiwa na umri wa miaka 37, ni moja ya sababu zitakazomfanya aonekane kuwa mmoja wa wachezaji bora kuwahi kuupamba mchezo huo. Mshindi huyo mara tano wa tuzo ya Ballon d'Or ndiye mchezaji pekee kwenye Ligi Kuu mwenye hat-trick mbili msimu huu.

Ya kwanza ilikuwa katika ushindi wa 3-2 dhidi ya Tottenham Hotspur.

Wiki moja iliyopita, alirudia ushujaa uleule, akiifungia Manchester United kwenye ushindi mwingine wa 3-2 dhidi ya Norwich.

Cristiano Ronaldo amefunga hat-trick ya 60 katika maisha yake ya soka (58 kwa ngazi ya klabu).

Ronaldo ni gwiji linapokuja suala la kufunga mabao matatu katika mechi moja. Mreno huyo anashikilia rekodi ya kufunga hat-trick nyingi zaidi kuliko mwanasoka yoyote karne ya 21 (60).


RONALDO

## Nukuu

"Nadhani haiwezekani tena kwetu kushinda ubingwa wa Ligi Kuu, lakini tutaweka nguvu tuwatoe kwenye Kombe la FA," **winga wa Simba, Bernard Morrison baada ya timu yake kutoka sare tasa dhidi ya Yanga**



"Nilijifunza mengi kutoka kwa Guardiola. Falsafa yake ni ya kusisimua; alichokifanya Barcelona, Bayern na sasa akiwa na Manchester City, mtindo huo wa kushambulia na kuvutia unamuona akishinda sana. Ni muundo huu ambao nimejaribu kuutekeleza nikiwa na Ajax," **Kocha ajaye wa Manchester United (kwa sasa Ajax), Erik ten Hag, ambaye alifanya kazi na Pep Guardiola wakiwa Bayern Munich.**



"Bado mechi tano [kabla ya mechi ya jana dhidi ya Leicester City] zimebaki na tunahisi kwamba tutalazimika kushinda zote ili kupata nafasi hiyo [ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya]. Tuna uwezo zaidi wa kufanya hivyo, tunaamini katika hilo na hilo ndilo tutajaribu kufanya. Je, bado iko mikononi mwetu? Ndio. Tukishinda mechi tano tutakuwa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, hivyo ndivyo tunavyopaswa kuiangalia," **mshambuliaji wa Tottenham, Harry Kane**



# 'DABI' YA KARIAKOO 2022 ILIYOWAPA MAKIPA LIKIZO



Winga wa Simba, Bernard Morrison, akimlamba chenga straika wa Yanga, Fiston Mayele kwenye mechi ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa juzi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na kumalizika kwa sare tasa. **NA MPIGAPICHA WETU**

**Na Adam Fungamwango**

DAKIKA 90 za mchezo wa watani wa jadi kati ya Simba na Yanga Jumamosi iliyopita, zilimalizika huku ikiwekwa rekodi ya moja kati ya mechi chache za timu hizo ambazo hazikuwa na mashambulizi ya maana.

**Kiufundi makocha wa timu zote mbili, Pablo Franco kwa upande wa Simba na msaidizi wa Nasreddine Nabi, Cedric Kaze wa Yanga, walijitahidi sana kujaza viungo kati ambako ndiko kulikuwa na vita, lakini mbele zilikuwa dhaifu mno.**

Dabi hii ilionekana kupooza, kwani hakukuwa na mashambulizi makali ambayo huwa yanashuhudiwa zinapopambana, pande zote zinapopata nafasi ya kwenda kushambulia, basi hushambuliana kwa nguvu mno.

Kuna wakati wachezaji wa pande zote mbili walionekana walioridhika tu, na walifurahia zaidi kupasiana kuliko kwenda kutafuta bao.

Wakati mwingine ilionekana ni kama bonanza, kwani wachezaji hawakuwa na kasi kama tulivyozoea kwenye dabi nyingi zinazojulikana.

Makipa wa pande zote mbili walionekana kuwa likizo isiyo na malipo, kwani hawakupata kashikashi za kuwatia majaribuni.

Inawezekana Aishi Manula wa Simba na Djigui Diarra wa Yanga wakawa walipata wakati mgumu kwenye mechi zingine za Ligi Kuu ambazo timu zao zimecheza kuliko hiyo ya juzi.

Kwa upande wa Simba yenyewe tangu kuanza kwa msimu huu haina kabisa mastraika wa maana, ambapo wale watatu iliyokuwa inawategemea, Meddie Kagere, John Bocco, na Chris Mugalu wanaonekana wamefikia ukingoni.

Na wala mashabiki hawatoshangaa kama wote wakiachwa msimu huu utakapomalizika.

Simba ilisimamisha straika mmoja Mugalu, ambaye kwenye Ligi Kuu mpaka sasa hajafunga goli lolote. Alipiga kichwa kimoja kilichodakwa na kipa Djigui Diarra, lakini muda mwingi wa mchezo hakuwa na madhara.

Ilivyoonekana ni kwamba kama Simba ingepata bao kwenye mechi hiyo, basi lingefunga na mchezaji wa kiungo au beki na si straika, kwani hata Bocco alipoingia dakika chache zilizobaki hakuna alichofanya zaidi ya kupiga faulo juu kabisa.

Yanga ina bahati msimu huu ya kuwa na straika hatari, Fiston Mayele ambaye naye juzi alidhibitiwa kikamilifu na beki wa Simba Mkongomani mwenzake, Henoc Inonga.

Baada ya Mayele kukamatwa, Yanga ilionekana haikuwa na njia yoyote ile iliyoonekana ya kupata bao, badala yake Jesus Moloko na Kibwana Shomari walikuwa wakipiga krosi ambazo hazikuwa na madhara yoyote ile.

### Takwimu za kusikitisha

Katika kuthibitisha kuwa 'dabi' ya juzi haikuwa kama vile ambavyo wengi walifikiria, Yanga haikupiga shuti lolote lile lililolenga lango. Hili ni tatizo kubwa hasa kwenye mechi kubwa kama hiyo.

Wala huwezi kusema kuwa labda mabeki wa Simba waliifanya kazi yao kwa asilimia 100, kuna wakati walifanya makosa, lakini Yanga ilishindwa hata kupiga shuti moja, Manula akadaka.

Yanga ilipiga mashuti matatu nje, mawili hayakuwa hatari, ni moja tu la Mayele ndiyo lililokuwa almanusura libadilishe mtazamo. Kama lingelenga lango, ingekuwa ni hatari mno, lakini liligusa nyavu za nje.

Kwa upande wa Simba ililenga lango mara mbili, moja kichwa kilichomlenga Diarra kilichopigwa na Mugalu, na Denis Kibu naye alipiga shuti baada ya kutokea kizaazaa langoni, lakini kipa akaudaka.

Ilipiga mashuti manne nje mbayo hayakuwa na hatari yoyote ile. Hivyo ndivyo ilivyoisha kwa suluhu kwenye mechi isiyokuwa na mvuto, iliyokosa ubunifu.

Kwa mara nyingine tena, mechi ya watani wa jadi Simba na Yanga msimu huu imeisha kwa bila kufungana na kugawana pointi moja moja. Kwa maana hiyo Simba na Yanga hazijafungana bao lolote, huku kila timu ikichukua pointi mbili kutoka kwa mwenzake.

Mechi ya mzunguko wa kwanza kwenye uwanja huo huo iliyochezwa Desemba 11, mwaka jana zilitoka pia bila kufungana.

### Mataifa tisa yalihusika

Kwenye mechi hiyo, ilikuwa na wachezaji kutoka jumla ya mataifa tisa ya Afrika ambao walishuka dimbani. Mataifa hayo ni Tanzania, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Ghana, Kenya, Mali, Senegal, Zambia, Uganda na Burundi.

Tukiwaacha wachezaji wa Kibongo ambao walikuwa wengi kwenye mechi hiyo, Djigui Diarra na Sadio Kanoute wao wanatoka nchini Mali, Joash Onyango (Kenya), Bernard Morrison (Ghana), Mayele, Inonga, Jesus Moloko, Yannick Bangala, Djuma Shaaban (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo).

Khalid Aucho yeye anatokea Uganda, Saido Ntibazonkiza (Burundi), Pape Shakho (Senegal), Clatous Chama na Rally Bwallya wao ni kutoka Zambia.

### Yanga ubingwa mweupe

Baada ya suluhu hiyo, kwa asilimia kubwa inaipa Yanga nafasi kubwa ya ubingwa, kwa kufikisha pointi 55, huku ikiwa bado haijapoteza mechi yoyote mpaka sasa.

Angalau Simba ndiyo iliyoonekana kuwa inaweza kutibua rekodi hiyo, lakini imeshindwa kufanya hivyo.

Kutokana na hilo, Yanga ina nafasi kubwa ya kuweza kumaliza Ligi Kuu bila kupoteza, lakini pia ipo karibuni zaidi ya ubingwa msimu huu.

Simba imefikisha pointi 42, pointi 13 nyuma ya vinara Yanga, lakini ikiwa na kiporo kimoja mkononi.

### JE, WAJUA?



MSHAMBULIAJI wa zamani wa Wales, Craig Bellamy, anashikilia rekodi ya kuzifungia klabu nyingi (7) tofauti za Ligi Kuu England, nyota huyo ambaye alianza kucheza Ligi Kuu nchini humo mwaka 2000 akiwa na Coventry City, kisha Newcastle (2001-2005), Blackburn Rovers (2005-2006), Liverpool (mara mbili kati ya 2006-2007 na 2011-2012), West Ham United (2007-2009), Manchester City (2009- 2011) na Cardiff City (mara mbili wakati wa msimu wa 2010–2011 kwa mkopo na 2012–2014), amestaafu akiwa amefunga jumla ya mabao 81 kwenye mechi 294 katika klabu saba tofauti.



# Yabaini utitiri leseni za uchimbaji madini

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Tanzania (TAKUKURU) mkoani Dodoma imebaini kuwapo utitiri wa leseni za uchimbaji za madini ya ujenzi hali inayosababisha upotevu wa mapato katika Halmashauri.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Mkuu wa TAKUKURU mkoani humo, Sosthenes Kibwengo alisema moja ya Halmashauri iliyoonekana kuwa na tatizo hilo ni Mpwapwa ambayo ina leseni za wachimbaji madini 773 lakini zinazotumika ni 57 huku nyingine zikikaa bila kutumiwa.

Kibwengo, alisema TAKUKURU ilibaini kuwapo kwa utitiri huo wa leseni za uchimbaji madini ya ujenzi lakini hakuna kinachoendelea katika maeneo mbalimbali na kupelekea kuzinyima mapato Halmashauri.

Hata hivyo, Kibwengo alisema Halmashauri zinapoteza mapato katika maeneo ambayo uchimbaji unafanyika kiholela pamoja na maeneo ambayo hayana mashine za kielektroniki za kukusanyia ushuru (POS).

Pia, Kibwengo alisema TAKUKURU imefuatilia utekelezaji wa miradi 41 yenye thamani ya Sh. bilioni 11.2 katika sekta za maji,ujenzi,elimu na afya.

Alifafanua kuwa katika miradi hiyo inajumuisha na ile ya Mpango wa Maendeleo wa Ustawi wa Taifa dhidi ya Mapambano ya UVIKO-19.

Alisema katika eneo hilo miradi 10 ambayo ni sawa na asilimia 24 ilikutwa na mapungufu madogo ikiwemo ya kucheleweshwa kukamilika kwa mujibu wa mkataba na kusababisha kuongezeka kwa gharama katika matumizi ya vifaa visivyokidhi ubora na manunuzi kwenye bei ya soko.

Kibwengo, alibainisha kuwa mradi mmoja ambao ulikuwa na viashiria jinai taasisi hiyo imeanza uchunguzi na kuongeza kuwa Sh. milioni 409.4 zilizolipwa kwa mkandarasi kinyume na taratibu katika utekelezaji wa mradi mmoja zilirejeshwa kwa ushirikiano wa Halmashauri husika.




Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma Prof Davis Mwamfupe akizungumza na madiwani wa jiji hilo (hawapo pichani) kwenye kikao cha Bazara la Madiwani kilichofanyika Dodoma juzi, (kushoto) Mkurugenzi wa Jiji Joseph Mafuru, (kulia) Naibu Meya wa Jiji, Emmanuel Chibago wa mwisho kulia ni Mwenyekiti wa CCM wilaya ya Dodoma mjini. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Baraza la Wawakilishi lakunwa miradi ya TBA

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati, imesema miradi ya ujenzi inayotekelezwa na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) jijini Dodoma, itasaidia kuishauri serikali ya Zanzibar kuweka mipango ya aina hiyo visiwani humo.

Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa jengo la Ofisi za Wizara zote za Zanzibar katika Mji wa Serikali Mtumba, ujenzi wa nyumba 500 za watumishi eneo la Nzuguni na nyumba za viongozi eneo la Kisasa.

Akizungumza mwishoni mwa wiki baada ya kutembelea miradi hiyo, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Yahya Rashid Abdallah alisema ziara hiyo inalenga kujifunza ili kuishauri serikali hususani katika kipindi hiki cha bajeti ya mwaka 2022/23.

"Dhamira yetu ni kuona mazuri yaliyofanyika bara hususani kwenye miradi mbalimbali ili tuige hasa katika utekelezaji wa miradi kwa upande wa Zanzibar, lengo letu ni kuona namna ambavyo wenzetu wanatekeleza shughuli zao za miradi, changamoto zao na jinsi wanavyozitatua, na kuelewa jinsi wanavyoshirikiana na taasisi za Zanzibar katika shughuli za kiutendaji,"alisema.

Alisema wamekuja kwenye ziara hiyo kipindi mwafaka kwa sababu ni kipindi cha bajeti na wameongozana na watendaji wa taasisi husika ili kujifunza.

"Utayari wa serikali katika na taasisi binafsi ni funzo kubwa ambalo tumelipata, tumeona jinsi wenzetu walivyotanguliza miundiombinu maana imeshawekwa tayari kwa ajili ya utekelezaji miradi husika, tunapaswa kwenda Zanzibar kurekebisha baadhi ya maeneo yetu ili kupata ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yatu,"alisema.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Joseph Kirangi alisema ziara hiyo itawasaidia wakati wanapotoa uelekeo, sera au miongozo ya serikali kwa upande wa Baraza la Wawakilishi.

Mkurugenzi wa Idara ya Ushauri kutoka TBA, Wancelaus Kizaba alieleza kuwa miradi inaendelea kwa kasi kubwa na lengo lao ni kukamilisha kwa wakati.

# Kongamano laipa serikali maazimio

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KONGAMANO la kitaifa la ufuatiliaji na tathmini limetoa maazimio tisa ili serikali kuyafanyia kazi ikiwamo kutungwa kwa sera ya masuala hayo.

Mkurugenzi wa Idara ya Uchambuzi na Ushauri wa Kazi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Nolasco Kipanda, aliyasoma maazimio hayo juzi jijini hapa katika kongamano hilo lililoandaliwa na Umoja wa Tathmini nchini (TanEA) na Ofisi hiyo.

Alisema washiriki wameomba Serikali kuangalia namna ya kuwa na sera ya ufuatiliaji na tathmini ili suala hilo kutoa nguvu ya kisheria.

Pia alisema wamehimiza uwapo wa ushirikiano kati ya Serikali na taasisi zake, wadau na kuishauri watoa waamuzi ili kutumia vizuri matokeo ya ufuatiliaji na tathmini.

"Kama tunataka kuona matokeo ya ufuatiliaji na tathimini matokeo ya we na evidence based ( yawe na ushahidi), washiriki wamesisitiza kuwa isionekane kuwa ufuatiliaji na tathmini unachukua nafasi ya ukaguzi ila ni vitu ambavyo vinasaidiana katika kuleta ufanisi,"alisema.

Alisema kuna haja ya Serikali kutambua na kuimarisha vya kutosha vitengo vya ufuatiliaji na tathmini na kupatikana kwa rasimali watu na fedha za kutosha.

"Washiriki wamesisitiza haja ya Serikali na sekta binafsi kuendelea kuangalia maeneo yenye changamoto katika masuala ya ufuatiliaji na tathimini ili yaweze kutafutiwa majawabu,"alisema.

Akifunga kongamano hilo, Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, Deogratias Ndejembi, alizitaka taasisi za Serikali kuimarisha ufuatiliaji na tathmini kwa lengo la kuimarishaji utendaji kazi wa taasisi.

Alisema ufuatiliaji na tathimini unasaidia kupata thamani na matumizi sahihi ya rasilimali na kuzitaka taasisi za Serikali kuimarisha jambo hilo. "Hoja na michango ambayo mmeitoa wakati wa majadiliano kwenye kongamano hili yatasaidia katika kuboresha eneo hili la ifuatiliaji na tathimini na kuwahakikishia kuyafanyia kazi yalie yaliyoibuliwa kwenye kongamano hilo."

"Kwa niaba ya Serikali niwahakikishie hoja na michango mliyoiwasilisha tutaifanyia kazi ipasavyo. Maana nimejulishwa katika hoja hizo kuna mambo mbalimbali ambayo mmeyagusiwa ikiwemo kuigeuzi masuala ya ufuatiliaji na tathimini kuwa kada kamili na kuwa na Bodi yake haya yote tunayachukua kwenda kuyafanyia kazi ili kuona tutafanya nini huko mbeleni,"alisema.





# Watatu wafariki kwa kusombwa maji, kuangukiwa kuta

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

WATU watatu wamefariki dunia na wengine kadhaa kujeruhiwa wilayani Kyela, kutokana na kusombwa maji na kuangukiwa na kuta za nyumba baada ya mafuriko yaliyosababishwa na mvua iliyonyesha katika wilaya za Rungwe na Ileje, kuvamia makazi yao.

Mito iliyokuwa imefurika ni Songwe ambao chanzo chake ni katika wilaya za Mbozi, Momba na Ileje mkoani Songwe, Mto Kiwira na Mbaka ambayo vyanzo vyake vipo katika Wilaya ya Rungwe pamoja na vijito vidogo vidogo.

Mafuriko hayo pia yamesomba mazao mashambani na majumbani na mifugo ya wananchi na kuharibu miundombinu ya barabara na madaraja na kukata mawasiliano kwenye baadhi ya maeneo.

Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya ilifanya ziara katika wilaya hiyo kwa ajili ya kuangalia hali ilivyo na kutoa misaada kwa baadhi ya waathirika waliohifadhiwa kwenye kambi mbalimbali wilayani humo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema awali walikuwa wamepata taarifa kwamba kulikua na watu wawili walifariki, lakini juzi wakapata taarifa kutoka kwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi wa wilaya hiyo kuwa vifo vimeongezeka.

Alisema watafanya mawasiliano na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kitengo cha Maafa ili kuwasaidia wananchi walioathirika na mafuriko hayo na Ofisi ya Mkoa kwa kushirikiana na ya Wilaya wataendelea kufanya tathmini.

Aliwataka wananchi hao waendelee kuwa na subira wakati serikali ikijipanga kuwasaidia hasa kwa vitu ambavyo vitatakiwa kutatuliwa kwa haraka ikiwamo upatikanaji wa chakula.

"Lakini tumepata taarifa kwamba kuna baadhi mmeanza kurejea kwenye maeneo yenu, nawaomba muendelee kuchukua tahadhari ili vifo visije vikaongezeka, lakini pia sisi tuna takwimu za nyumba zote ambazo zimeathirika kwahiyo tutaendelea kushughulikia tatizo hili kwa dharura," alisema Homera.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maafa ya Wilaya ya Kyela, Ezekiel Magehema, alisema mafuriko hayo yameathiri nyumba 498 ambazo kati yake 249 zimebomoka na zingine 249 zimeharibika kiasi na kusababisha kaya 234 kukosa makazi.

Alisema mafuriko hayo yaliharibu hekta 10,616 za mpunga na mazao mengine, kusomba ng'ombe 101, nguruwe 200 na kuku 2,061 za wananchi katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo.

Magehema alisema kati ya kata 33 za Wilaya ya Kyela, Kata 15 ziliathiriwa na mafuriko hayo ambazo ni Kata ya Katumba Songwe, Mababu, Mwaya, Kanjunjumele, Bujonde, Ndandalo, Mkuyu, Ikolo na Ikama.

Alizitaja kata zingine kuwa ni Talatala, Njisi, Ipinda, Makwale, Ndobo na Kata ya Matema na kuwa baadhi ya kata hizo ziliguswa kwenye maeneo machache.

"Aprili 27 na 28 shule za msingi 27 na sekondari tano hazikuendelea na masomo kutokana na mafuriko hayo, maeneo ziliko shule hizo yalikuwa hayafikiki," alisema Magehema.

Alisema kwa sasa wanaendelea na tathmini ya kila kijiji kwa kushirikiana na viongozi wa ngazi zote ili kujua athari halisi za mafuriko hayo.

Nipashe lilitembelea baadhi ya maeneo yaliyoathirika na kushuhudia nyumba za wananchi zikiwa zimebomoka na zingine zikiwa zimejaa maji na matope huku baadhi ya wananchi wakisema mafuriko hayo yalileta nyoka wakali kwenye makazi yao.

Wilaya ya Kyela huathiriwa na mafuriko kila mwaka na asilimia kubwa ya mafuriko hayo husababishwa na mvua inayonyesha katika wilaya za Rungwe na Ileje.



Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya (kushoto) akitoa maelekezo kwa Meneja wa Wakala wa Barabara (Tanroads) mkoa wa Songwe, Mhandisi Suleiman Bishanga, alipotembelea na kukagua barabara inayounganisha kata ya Isongole, Ibungu, Katengele, Lubanda kwenda Keikei, zilizopo wilaya ya Ileje, mkoani humo. **PICHA: WIZARA YA UJENZI**

# Wenye ulemavu wapata mkopo mil. 130/- bila riba

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya imetoa mkopo usio na riba wa zaidi ya Sh. milioni 130 kwa vikundi vya watu wenye ulemavu ili waweze kuendeleza shughuli zao za ujasiriamali na kujiinua kiuchumi.

Mkopo huo ni utekelezaji wa sheria za nchi zinazoitaka kila halmashauri nchini kutenga asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kukopesha vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili kuendeleza shughuli zao.

Mikopo hiyo imetolewa kwa vikundi 17 vya watu wenye ulemavu katika kipindi cha miaka miwili ambayo ni mwaka wa fedha 2020/2021 na 2021/2022.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya ya Mbarali, Roman Kessy, aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na Nipashe kuhusu hali ya utoaji wa mikopo hiyo katika halmashauri hiyo na manufaa yake kwa wananchi.

Alisema mikakati waliyoweka kama wilaya ni kuhakikisha vikundi vyote vya watu wenye ulemavu vinapata mikopo na kurejesha kwa wakati pamoja na kufuatilia mabadiliko yanayosababishwa na mikopo hiyo.

Alisema ili kuhakikisha fedha hizo zinarejeshwa waliamua kuweka utaratibu wa kutoa fedha kidogo kidogo kwa vikundi hivyo ili kuwapima wahusika kama wanaweza kuwa waaminifu.

"Inachofanyika ni umakini mkubwa kwa kadri timu ya upembuzi wa mikopo itakavyoona inafaa, ipo timu maalumu ambayo inafuatilia vikundi hivi na kuhakikisha vinarejesha mikopo hii kwa wakati, kwenye hili tumefanikiwa," alisema Kessy.

Alisema vigezo wanavyoangalia wakati wa kutoa mikopo hiyo ni kuangalia watu wenye ulemavu wenye uwezo wa kufanya shughuli yoyote ya uzalishaji mali ikiwamo biashara ambayo inaonekana.

Kessy alisema katika kuhakikisha watu wenye ulemavu wanafanya biashara zao vizuri baada ya kupatiwa mikopo, elimu ya ujasiriamali imekuwa ikitolewa kwa watu wenye ulemavu ikiwamo kutambua masoko ya bidhaa zao.

Baadhi ya watu wenye ulemavu ambao wamenufaika na mikopo hiyo walisema wanaishukuru serikali kwa kuanzisha utaratibu huo wa mikopo wakieleza kuwa imewasaidia kuinuka kiuchumi.

Mmoja wa wanufaika hao, Maria Daudi, alisema baada ya kupata mkopo huo katika kikundi chao, aliamua kufanya biashara ya mchele katika stendi ya Igurusi na kupitia biashara hiyo amepata maendeleo tofauti na ilivyokuwa awali.

Alisema anapata fedha kwa ajili ya kuendeshea maisha na familia yake na kurejesha mkopo huo kila mwezi, sasa anaelekea kumaliza kurejesha mkopo.

"Huu mkopo umenisaidia sana mimi na familia yangu maana nina watoto ambao ninasomesha mwenyewe na mume sina hivyo nazingatia maelekezo niliyopewa na wataalamu, nazingatia urejeshaji kwa wakati ili na wengine wakope," alisema Maria.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Twalib Lubandamo, alisema kuwa halmashauri baada ya kutoa mikopo hiyo kwa vikundi vya watu wenye ulemavu huendelea na ufuatiliaji wa kina.

"Ingawa baadhi ya vikundi hivi huwa vinatusumbua baada ya kupatiwa mikopo wakidhani wamepewa kama zawadi, tunawashauri warudishe kwa wakati wasisubiri ufuatiliaji au kufungiwa biashara zao," alisema Lubandamo.

Diwani wa kata ya Rujewa, Jeremiah Makao, alisema katika kata yake kuna wenye ulemavu wanaojituma kufanya kazi huku wengine wakichukua mikopo ya halmashauri.

## Vijana 178 walioacha masomo warudishwa shuleni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imesema imefanikiwa kuwarejesha kuendelea na masomo ya elimu ya sekondari vijana 178 walioacha shule kwa sababu mbalimbali ikiwamo kupata mimba ambao wanasoma katika shule mbalimbali.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema vijana hao wanaendelea na masomo katika shule mbalimbali za sekondari za serikali mkoani humo ambazo ziliandaliwa maalumu kwa ajili ya kupokea kundi hilo.

Vilevile, alisema kuwa serikali imetoa Sh. bilioni 3.29 kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari saba katika halmashauri zote za Mkoa wa Mbeya, lengo likiwa ni kuboresha kiwango cha elimu na kuhakikisha watoto wote walioacha masomo wanapata elimu

"Rais wetu amefanya kazi kubwa sana katika mkoa wetu wa Mbeya katika nyanja mbalimbali hususan sekta ya elimu kwa kuona vijana waliokosa fursa ya elimu wanarejeshwa shuleni ikiwa ni pamoja walioacha masomo kutokana na mimba," alisema Homera.

Aliyataja matatizo makubwa yanayosababisha wanafunzi wengi kuacha shule kuwa ni pamoja na mimba za utotoni, kufiwa na wazazi pamoja na unyanyasaji kwenye ngazi ya familia.

Homera alisema kuwa katika kuboresha sekta ya elimu pia Vijana 1,265 wamepata fursa ya kuendelea na elimu ya masomo ya ufundi stadi kupitia vyuo vya Ufundi stadi (VETA) ambayo yanatolewa chini ya udhamini wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa upande wake, Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya, Dk. Angelina Lutambi, alisema katika kipindi cha mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan, mkoa umepokea zaidi ya Sh. bilioni 64.8 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo hususan sekta ya elimu msingi na sekondari.

Alisema, pia sekta zingine kama afya, miundombinu ya barabara na sekta ya kilimo zimenufaika kwa miradi mbalimbali kutekelezwa ndani ya mkoa huo.

"Mkoa wetu ni miongoni mwa iliyonufaika na miradi mbalimbali ya maendeleo, ipo miradi imetekelezwa kwa kutumia fedha za Uviko-19, fedha za tozo na miradi mingine, kwahiyo wananchi lazima wawe na imani na serikali yao," alisema Dk. Lutambi. Aliwataka wananchi wa mkoa huo kuendelea kushirikiana na serikali kwenye utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo inayotekelezwa kwenye maeneo yao.





Mkurugenzi Mkuu wa Bank of Africa (BOA), Adam Mihayo (kushoto) akisalimiana na mmoja wa wateja wakati wa Iftar iliyoandaliwa na Benki hiyo kwa wateja wake mjini Zanzibar mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yasikia kilio cha w'biashara Darajani

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema kwamba serikali imezisikia kero na changamoto za wafanyabiashara katika eneo la kitovu cha Biashara Darajani mjini Zanzibar.

Othman aliyasema hayo jana baada ya kukamilisha ziara yake katika maduka mbalimbali yanayouzwa bidhaa za mahitaji ya sikukuu kuona hali halisi ya bei hizo katika mitaa ya Mlandege, Mbuyuni, Mchangani na Darajani mjini Zanzibar.

Miongoni mwa changamoto zilizobainika ni pamoja na upandaji wa bei za bidhaa mbalimbali zikiwamo nguo za kike na kiume, viatu, mashuka, ambazo ndiyo mahitaji muhimu katika kipindi cha kuelekea Sikukuu ya Eid-el fitri inayotarajiwa kuanza kesho.

Alisema wafanyabiashara katika maeneo ya maduka mengi aliyopita wamelalamikia upandaji wa bei ya bidhaa mbalimbali hasa zinazotumika kwa mahitaji ya sikukuu kutokana na sababu tofauti ikiwamo ya kupanda kwa gharama za usafirishaji.

Alisema baadhi ya wafanyabiashara wamedai katika kipindi cha nyuma walikuwa wakisafirisha kontena moja la viatu kwa gharama ya Dola za Marekani zipatazo 5,000 ambazo ni karibu Sh. milioni 12 za Tanzania.

Hata hivyo, alisema hivi sasa kontena hilo hilo linasafirishwa kwa wastani wa Dola za Marekani 13,000 ambazo ni ongezeko la karibu Dola 8,000 ambao ni mzigo wa gharama unaokwenda kwa wananchi na watumiaji wengine wa bidhaa hizo.

Alisema wafanyabiashara wamekuwa wakitoa sababu tofauti zinazochangia bei ya gharama hizo kupanda ikiwemo ya mlipuko wa maradhi ya corona na vita vinavyoendelea Ukraine.

Vile vile, alisema wapo wafanyabiashara wanaodai kupanda na kuongezeka kwa gharama za kodi na upatikanaji wake ikiwamo namna ya wasimamizi wa ndani wa kodi ambao wanaonesha sio rafiki na hawazingatii hali halisi ya biashara ya ndani.

Alisema, wafanyabiashara wametoa mfano wa tathmini ya malipo ya kodi inayofanywa katika kipindi cha ramadhani, lakini ikatumika katika kipindi cha meizi mingine jambo ambalo linasababisha mzigo kwao kuongezeka kwa kuwa hakuna uwiano sahihi katika harakati za kibiashara Zanzibar.

Mapema baadhi ya wafanyabiashara walimueleza, Makamu kwamba bado Zanzibar wanakabiliwa na changamoto ya kulipa kodi kwa woga na watumishi wa mamlaka za kodi sio rafiki na wengi wao wanatumia vitisho jambo ambalo linakwaza harakati za biashara.

## ... Yasema hakuna urasimu fedha za maendeleo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Saada Mkuya Salum, amesema hakuna urasimu unaofanywa na ofisi yake katika utoaji wa fedha kwa ajili ya maendeleo bali kinachohitajika ni kufuata utaratibu.

Aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akitoa ufafanuzi kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuhusu maombi ya fedha ya zaidi sh. bilioni 1.3 zilizoombwa kwa ajili mkandarasi aliyekuwepo katika kituo cha Kidimni.

Alisema maombi ya fedha hizo tayari yapo katika utaratibu wa kutoka, lakini kuna baadhi ya matakwa ambayo mamlaka ya kudhibiti dawa za kulevya walitakiwa kuwasilisha na tayari wameshawasilisha.

Aidha, alisema ofisi hiyo ni msimamizi wa fedha za umma sio fedha zake na hakuna mtu anaeweza kufanya atakavyo mwenyewe bali jambo linalofanywa kuhusiana na fedha za umma, matumizi yote yanakwenda kwa mujibu wa utaratibu.

"Ni lazima utaratibu ufuatwe fedha zipo na mkandarasi abakie katika eneo la kazi na fedha zitatoka kwa mujibu wa taratibu hii ni fedha ya umma ni lazima utaratibu ufuatwe kwa tasisi yoyote ile na sio fedha ya mtu yoyote," alisisitiza.

Alisema ni lazima utaratibu ufuatwe katika fedha hizo ambazo zimo katika sheria walizozitunga katika chombo hicho muhimu cha Baraza la Wawakilishi.

Alizungumzia pia hoja ya fedha Sh. milioni 24 ambazo zimewekwa kwenye programu ya udhibiti wa dawa za kulevya hasa katika kudhibiti usambazaji na usafirishaji wa dawa za kulevya.

# Marufuku kupiga muziki kwenye viwanja sikukuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIKA kuelekea sherehe za Sikukuu ya Eid-el-fitri, Serikali ya Mkoa wa Kaskazini Unguja imepiga marufuku upigaji wa muziki katika viwanja mbalimbali vya kusheherekea sikukuu hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari Mkuu wa mkoa huo, Ayoub Muhamed Mahmoud, alisema kuwa ni marufuku kupiga muziki katika viwanja vya wazi vya kusheherekea sikukuu.

Alisema kuwa mkoa huo ni ukanda wa sekta ya utalii na kuwataka wamiliki wa hoteli za kitalii ambao wanakumbi za starehe kuhakikisha kuwa wanafuata masharti yaliyowekwa na serikali ya mkoa huo.

Alisema miongoni mwa taratibu hizo ni kuhakikisha wanaopiga muziki mwisho ni saa sita usiku na kuhakikisha kuwa hauwabuguzi watu wengine.

Mkuu wa mkoa huyo alikabidhi vyakula kwa ajili ya Sikukuu ya Iddi kwa wananchi wa mkoa huo ambavyo vimetolewa na taasisi ya Aviation Service Management.

Kwa upande wake Jeshi la Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, limesema kuwa litahakikisha linaimarisha ulinzi katika kipindi chote cha sikukuu hiyo ili kuhakikisha wananchi wanasherehekea kwa amani na usalama.

Kaimu Kamanda wa Polisi mkoa huo, Elisante Makiko Mmary, alisema jeshi hilo limejipanga vyema ili kuhakikisha linadhibiti na kupambana na matukio yote ya kihalifu na wahalifu ambao wanatumia nafasi ya sikukuu kufanya uhalifu katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

Aidha alisema jeshi hilo limejipanga kuweka ulinzi katika viwanja vyote vya sikukuu pamoja na kufanya doria katika fukwe za bahari na maeneo yote ya mkoa huo ili kuhakikisha wananchi wanasherehekea sikukuu hiyo kwa hali ya amani na utulivu.

"Tumeweka askari wetu wakaguzi katika shehia zote kwa ajili ya kulinda usalama wa wananchi wetu na niwahakikishie wawe huru katika kusherehekea iddi yao," alisema.

Aliwataka wazazi na walezi kutowaachia watoto peke yao kwenda kwenye viwanja vya sikukuu bila ya uangalizi wao.

Alisisitiza kwamba jeshi halitasita kumchukulia hatua kali za kisheria mzazi au mlezi yeyote ambaye atabainika kumuachia mtoto wake kwenda peke yake.

Hata hivyo, aliwataka wazazi kuhakikisha inapofika saa 12:00 jioni wanaondoka katika maeneo yote ya fukwe za bahari na kuwasisitiza wenye kumbi za starehe na viwanja vya sikukuu ni marufuku kupiga marufuku kupiga disko toto na kuheshimu muda uliopangwa na serikali wa kufungua na kufungua viwanja na atakaekwenda kinyume basi atachukuliwa hatua za kisheria.

Alitoa onyo kwa madereva wa gari za abiria na binafsi na vyombo vya maringi mawili kuchukua tahadhari na kuzingatia sheria za usalama barabarani ikiwamo kutoendesha vyombo hivyo kwa mwendo kasi, kutozidisha abiria kupitia kiwango kilichowekwa na mamlaka husika.

Kaimu Elisante aliwaasa madereva kuacha kuendesha vyombo vya moto wakiwa wamelewa, kuvaa kofia ngumu na kuacha kupiga misere ili kuepusha ajali zisizokuwa za lazima.

# Mgogoro KKKT waanza kufukuta upya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MGOGORO wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Konde, umeanza kufukuta upya baada ya wachungaji na vijana wanaomuunga mkono Askofu wa Dayosisi hiyo, Dk. Edward Mwaikali kutangaza misimamo mikali.

Wafuasi hao wameandaa waraka maalumu ambao wameuelekeza kwa Mkuu wa Kanisa hilo, Dk. Fredrick Shoo, wakimtaka aanze upya kusuluhisha mgogoro huo kabla ya kuendelea na mchakato wa kumuweka wakfu Askofu mpya wa Dayosisi hiyo, Geofrey Mwakihaba.

Mwenyekiti wa Idara ya Vijana wa Dayosisi hiyo, Jimbo la Mbeya Magharibi, Emmanuel Kaphace, alisema kwa mujibu wa Katiba ya KKKT Dayosisi ya Konde mkutano mkuu uliofanyika Machi 22, mwaka huu ulikuwa ni batili.

Alisema hata uchaguzi uliofanyika wa kumchagua Askofu Mwakihaba ni batili na hivyo wao bado wanamtambua Askofu Mwaikali kuwa ndiye kiongozi mkuu wa Dayosisi hiyo.

Alisema Idara ya vijana ya Dayosisi hiyo inamtaka Askofu Dk. Shoo kurejea katika Dayosisi hiyo kwenda kusuluhisha pande mbili zinazogombana akisema awali kiongozi huyo alisikiliza upande mmoja kabla ya kufanya uamuzi.

Kaphace alisema kwa mujibu wa Katiba ya KKKT uchaguzi wa Askofu unatakiwa kuandaliwa na Halmashauri Kuu ya Dayosisi na siyo Mkuu wa Kanisa kama ambavyo Dk. Shoo alifanya kwenye uchaguzi wa kumchagua Askofu Mwakihaba.

"Tunataka Mkuu wa Kanisa Dk. Shoo atujibu maswali yafuatayo, kuvunja katiba ya KKKT ni kosa ama sio kosa? Ni nani msimamizi wa Katiba ya Dayosisi ya Konde? Ni nani anatakiwa kuandaa uchaguzi wa Askofu wa Dayosisi ya Konde na Askofu Mwakihaba alichaguliwa ama aliteuliwa?" Alihoji Kaphace.

Alisema katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika Mwaka 2017, Mwakihaba alikuwa miongoni mwa wagombea waliokuwa wanashindana na Askofu Mwaikali na alishindwa kwa kura lakini baadaye akachaguliwa kuwa msaidizi wa askofu. Alisema wakati wa mchakato wa kuhamisha makao Makuu ya Dayosisi kutoka Tukuyu Mjini kwenda jijini Mbeya, Mwakihaba alishiriki, lakini baadaye akajiuzulu na kwenye uchaguzi ulioitishwa na Askofu Shoo wakamchagua kuwa Askofu wa Dayosisi hiyo kinyume na utaratibu.

Alisema wamebaini kuwa Askofu Dk. Shoo ndiye chanzo cha migogoro ndani ya Dayosisi hiyo kwa maelezo kuwa alikuwa mbali na dayosisi hiyo pia amesababisha migogoro mingine kwenye Dayosisi zingine za Kanisa hilo.

Kwa upande wao wachungaji wa Kanisa hilo wanaomuunga mkono Askofu Mwaikali walisema wao msimamo wao ni kuendelea kufanya kazi ya Mungu bila kuyumba mpaka mgogoro huo utakapokuwa umekwisha huku wakiomba Serikali Kuu Kuingilia kati.

Akisoma taarifa ya wachungaji hao, Mchungaji wa Ushirika wa Mbalizi Uswege Mwamasinga alisema kiini cha mgogoro wa Dayosisi hiyo ni ubadhirifu uliokuwa umefanywa na baadhi ya waliokuwa viongozi wa kanisa hilo.

Alisema viongozi hao walikuwa wamekopa fedha benki kwa ajili ya upanuzi wa Chuo Kikuu cha Tumaini Mbeya lakini fedha hizo zikapotea katika mazingira ya kutatanisha na kwamba wanaompinga Dk. Mwaikali wanataka kuuza baadhi ya mali za Kanisa hilo ili kulipa deni hilo.

"Askofu Dk. Mwaikali pamoja na wachungaji tumesimama kwa umoja wetu, hakuna mali ya kanisa itakayouzwa kulipa deni hilo, wachungaji tulitegemea Askofu Shoo angewakutanisha wachungaji wote wa Dayosisi ya Konde kwa ajili ya upatanisho," alisema Mwamasinga.

Alisema kwa mujibu wa Katiba ya Dayosisi ya Konde Toleo la Mwaka 2006, Askofu Mwaikali bado ni askofu wa Dayosisi ya Konde na kwamba uchaguzi uliofanyika ni batili na hata sherehe za kumuweka wakfu askofu Mwakihaba ni batili.



Sehemu ya wageni waalikwa pamoja na wafanyakazi wa Benki ya Exim waliohudhuria hafla ya futari iliyoandaliwa na benki hiyo kwa ajili ya wateja wake jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zaidi ya mil. 300/- zanunua boti za uvuvi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imenunua boti 16 na injini 12 zenye thamani ya Sh. milioni 395 zitakazotumiwa na maofisa uvuvi katika kudhibiti rasilimali za uvuvi nchini.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alisema hayo jijini Mwanza alipokuwa akizungumza kwenye hafla ya kukabidhi boti kwa maofisa wafawidhi wa uvuvi kwa Kanda za Ziwa Victoria, Tanganyika, Kanda ya Bahari ya Hindi, Kaskazini Mashariki na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Waziri Ndaki alisema boti na injini hizo zimenunuliwa na serikali ili kuiwezesha wizara na watalaam wake kutekeleza jukumu lake la msingi la kusimamia, kulinda na kuendeleza rasilimali za uvuvi nchini. Aliziomba halmashauri zote nchini kutenga bajeti kwa ajili ya kununua vifaa hivyo ili kudhibiti rasilimali za uvuvi dhidi ya watu wanaojihusisha na uvuvi haramu.

"Halmashauri zetu zilizo kwenye mwambao wa bahari/ziwa na mito zishirikiane na wizara ili kwa pamoja tudhibiti uvuvi haramu ambao bado ni changamoto kwa sasa," alisema.

Pia, alisema serikali itawashughulikia wavuvi haramu wote na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria.

Aliwataka wavuvi nchini kuhakikisha kuwa wanalinda rasilimali za uvuvi ili zisiharibiwe na watu wanaojihusisha na shughuli za uvuvi haramu.

Aliwataka maofisa uvuvi waliokabidhiwa boti na injini hizo kuzilinda na kuzitumia kwa malengo yaliyokusudiwa.

Awali, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) Dk. Rashid Tamatamah, alisema shughuli za uvuvi nchini hufanyika katika maji baridi na bahari na kiasi kikubwa zikihusisha wavuvi wadogo.

Alisema mwaka 2021 wavuvi wadogo 194,804 walishiriki moja kwa moja katika shughuli za uvuvi kwa kutumia vyombo vya uvuvi 57,991 na kuwezesha kuvuna tani 477,019 za samaki zenye thamani ya Sh. trilioni 2.8 na tani 302,827.9 sawa na asilimia 63.0 zilitoka Ziwa Victoria.

Vilevile, uvuvi huo ulihusisha tani 42,302 na samaki hai wa mapambo 181,268 zenye jumla ya thamani ya Sh. bilioni 414.23.

Dk. Tamatamah amefafanua kuwa ili uzalishaji wa samaki pamoja na mapato yake kwenye ziwa hili yawe endelevu, ajira zinazotokana na shughuli za uvuvi kwenye ziwa ziwe endelevu, miundombinu ya uvuvi iliyowekezwa na serikali na watu binafsi iweze kufanya kazi kwa muda mrefu na manufaa yatokanayo na shughuli za uvuvi kwenye ustawi wa jamii yawe endelevu, wananchi hawana budi kulinda na kuzisimamia ipasavyo rasilimali za uvuvi pamoja na mazingira zinakofanyika shughuli za uvuvi.

Alisema katika juhudi za wizara kusimamia rasilimali za uvuvi, iliunda kanda kuu nne za usimamizi wa rasilimali za uvuvi ambazo ni Kanda ya Ziwa Victoria, Kanda ya Ziwa Tanganyika, Kanda ya Bahari ya Hindi na Kaskazini Mashariki na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini zenye jumla ya vituo 36 vya Ulinzi na Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel ameipongeza Wizara ya Mifugo na uvuvi kwa hatua hiyo ya kununua vifaa hivyo ambavyo vitasaidia katika kudhibiti na kupambana na wavuvi haramu mkoani Mwanza na nchini kwa ujumla.

Akitoa shukurani kwa niaba ya maofisa ufawidhi wa uvuvi walipokea vifaa hivyo, Ofisa Mfawidhi kutoka Kanda ya Bahari Hindi na Kaskazini Mashariki, Mathayo Werema, aliishukuru serikali kwa ununuzi wa vifaa hivyo ambavyo watavitumia katika kudhibiti, kulinda rasilimali za uvuvi, pia kutoa elimu kwa jamii kuondokana na vitendo vya uvuvi haramu.

# Watakiwa kujiandaa uwekezaji gesi asilia

**Na Said Hamdani,** LINDI

TIMU ya Taifa ya Majadiliano kati ya Serikali na wawekezaji Mradi wa Gesi Asilia (LNG), imefanya ziara mkoani hapa na kuwataka wananchi kupokea fursa hiyo ya uwekezaji kwa kufanya maandalizi yakiwamo ya elimu na mahitaji mengine, ujenzi utakapoanza rasmi.

Ujumbe huo wa watu tisa akiwemo Gavana wa Benki Kuu, Profesa Florens Luoga, ulioongozwa na Mwenyekiti, Mhandisi wa Mafuta na Petroli, Charles Sangweni, uliwasili mjini hapa na kuona eneo lililotengwa kwa mradi husika na kufanya mazungumzo na uongozi wa mkoa.

Mwenyekiti Sangweni akizungumza na uongozi huo, alisema lengo la ziara ni pamoja na kuona eneo lililotengwa na jamii walivyojiandaa kuupokea mradi huo mkubwa kwa ukanda wa Afrika.

Alisema kutokana na umuhimu mkubwa wa mradi huo, Rais aliunda Timu ya Taifa ya majadiliano kati ya serikali na kampuni tano zilizojitokeza kuwekeza zikiongozwa na Equinor, Erizon na Shell.

Sangweni alisisitiza viongozi wa mkoa huo, majadiliano yakiendelea kufikia mwishoni ni vyema wakawahamasisha wananchi kuanza kujiandaa kielimu na mambo mengine ya uzalishaji wa mazao ili uwekezaji utakapoanza uwakute wameshajiweka katika nafasi nzuri.

"Kama mnavyofahamu kazi ya gesi ni ya kitaalamu, hivyo watahitajika watu walio na elimu na mahitaji mengine ikiwamo vyakula na vitoweo," alisema.

Pia, alisema majadiliano kati ya serikali na wawekezaji yaliyoanza mwaka 2016 na kuendelea 2018 na 2021 yanaenda vizuri na yanatarajia kufikia ukingoni.

Alisema kipindi cha ujenzi wa kiwanda utakapoanza unatarajiwa kuchukua muda wa kipindi cha miaka mitatu hadi mitano kukamilika kwake, huku kikitarajia kuchukua wafanyakazi, wakiwamo vibarua kati ya 10,000 hadi 15,000.

HABARI KIMATAIFA

## Morocco, Kenya zapaisha mishahara zaidi

**Rabat,** MOROCCO

SERIKALI ya Morocco imetangaza mipango ya kuongeza kima cha chini cha mishahara ya watumishi wa umma kwa asilimia 16 na kile cha wafanyakazi wengine kwa asilimia 10.

Ongezeko la asilimia 10 litapunguzwa kwa muda wa miaka miwili, ikishuhudiwa ongezeko la asilimia tano, Septemba mwaka huu na lingine, mwakani, kwa mujibu wa Morocco World News.

Ongezeko hilo lililopendekezwa lilikuwa sehemu ya makubaliano kati ya serikali, vyama vya wafanyakazi na shirikisho la waajiri.

Wananchi pia wataona ongezeko la posho za familia kwa wale wenye watoto zaidi ya watatu.

Wakati huo huo, Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta ameongeza kima cha chini cha mishahara kwa wafanyakazi kwa asilimia 12, kuanzia Mei Mosi, mwaka huu.

Rais Uhuru alitoa tangazo hilo jana, alipoongoza Wakenya kusherehekea Siku ya Wafanyakazi Duniani, katika uwanja wa Nyayo jijini Nairobi. **BBC**

## Doumbouya kuongoza Guinea miezi 39

**Conakry,** GUINEA

KIONGOZI wa Kijeshi wa Guinea, Kanali Mamady Doumbouya ametangaza kipindi cha miezi 39 cha utawala wa mpito, kabla ya nchi hiyo kurejea katika uongozi wa kiraia, akisema pendekezo la muda huo litawasilishwa bungeni.

Tangazo la kiongozi huyo mwanajeshi lilitolewa baada ya kuundwa kwa kile ambacho mamlaka nchini Guinea 'ilikiita mfumo shirikishi wa mashauriano, Aprili, mwaka huu.

Mchakato wa kuunda mfumo huo ulimalizika kwa kususiwa na makundi maarufu ya upinzani nchini humo.

Ijumaa iliyopita, baraza la mawaziri linalodhibitiwa na wanajeshi lilisema jukwaa lilioujadili mfumo huo lilitafakari uwezekano wa kuweka kipindi cha uongozi wa mpito cha kati ya miezi 18 na 52.

Katika hotuba yake, Kanali Doumbouya alisema muda wa miezi 39 aliouridhia ni wastani wa mapendekezo yaliyofikiriwa.

Jumuiya ya kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS), wiki iliyopita iliweka muda wa mwisho kwa serikali ya kijeshi ya Guinea kutangaza ratiba inayokubalika' ya kuondoka katika utawala wa mpito, la sivyo ikabiliwe na vikwazo vya kiuchumi na kifedha. **DW**

# Familia ya Rusesabagina yafungua kesi dhidi ya Rwanda

**Washington,** MAREKANI

FAMILIA ya Paul Rusesabagina, mhusika mkuu wa filamu iliyoshinda tuzo ya Oscar, iitwayo Hotel Rwanda, imewasilisha kesi nchini Marekani kuhusu madai ya kutekwa nyara na kuteswa kwa Dola milioni 400.

Rusesabagina, alihukumiwa kifungo cha miaka 25 jela kwa ugaidi na mahakama ya Rwanda mwaka jana katika kile ambacho wafuasi wake walikiita kesi ya uongo.

Familia yake inasema serikali ya Rwanda ilimrubuni kutoka Texas, alikokuwa akiishi uhamishoni, kurudi Rwanda.

Anasifiwa kwa kuokoa watu 1,200 wakati wa mauaji ya kimbari ya 1994.

Katika taarifa yake, familia ya Rusesabagina iliishutumu serikali ya Rwanda na maofisa wa ngazi za juu kwa kula njama ya kuwezesha na kutekeleza njama ya kumrubuni Rusesabagina kutoka nyumbani kwake San Antonio hadi Rwanda, ambako angeteswa na kuzuiliwa kinyume cha sheria kwa muda uliosalia wa maisha yake.

**Filamu ya Hollywood, Hotel Rwanda, ilitengenezwa mwaka wa 2004, na kumshirikisha Don Cheadle kama Rusesabagina.**

Taarifa hiyo iliongeza kuwa Dola milioni 400 ni kama fidia na itaongezeka kila siku ambazo Paul Rusesabagina anashikiliwa kifungoni. Malalamiko hayo yaliwasilishwa Washington DC, taarifa hiyo ilisema, na imewasilishwa kwa serikali ya Rwanda, ambayo bado haijatoa maoni hadharani.

Mauaji ya halaiki ya Rwanda yalidumu siku 100 kuanzia Aprili mwaka 1994, wakati watu 800,000, wengi wao kutoka kabila la Watutsi, wakiuawa na watu wenye itikadi kali kutoka jamii ya Wahutu.

Rusesabagina, meneja wa filamu hiyo, wakati huo, aliwalinda watu 1,200 kutokana na ghasia, baada ya kutafuta makazi katika jengo hilo.

Filamu ya Hollywood, Hotel Rwanda, ilitengenezwa mwaka wa 2004, na kumshirikisha Don Cheadle kama Rusesabagina.

Mwaka uliofuata alitunukiwa Nishani ya Urais ya Uhuru na Rais wa wakati huo wa Marekani George W Bush kwa juhudi zake.

Lakini safari ya Rusesabagina ikawa kutoka ubinadamu hadi adui wa taifa la Rwanda ilitokea huku ukosoaji wake kwa serikali ya baada ya mauaji ya kimbari na Rais Paul Kagame kupata hadhira kubwa.

Katika ujumbe wa video wa 2018, Rusesabagina alitoa wito wa mabadiliko ya utawala, akisema

"Wakati umefika kwa sisi kutumia njia zozote zinazowezekana kuleta mabadiliko nchini Rwanda".

Alikamatwa mwaka wa 2020, kwa mujibu wa wafuasi wake, ndege binafsi ambayo aliamini ingempeleka Burundi, badala yake, ilitua katika mji mkuu wa Rwanda, Kigali.

Septemba mwaka jana, alipatikana na hatia ya kuunga mkono kundi la waasi lililoendesha mashambulizi mabaya mwaka 2018 na 2019 nchini Rwanda.

Wakati huo, Marekani, ambako Rusesabagina ni mkazi, ilisema ina wasiwasi na hukumu hiyo. **BBC**



Rais Uhuru Kenyatta akihutubia wakati wa maadhimisho ya sherehe za Siku ya Wafanyakazi Duniani, katika uwanja wa Nyayo, nchini humo, jana. **PICHA: MTANDAO**

# Video za ngono zamng'oa mbunge bungeni

**Devon,** UINGEREZA

NEIL Parish amesema anajiuzulu kama mbunge baada ya kukiri kuwa alitazama ponografia mara mbili akiwa bungeni.

Parish, ambaye amewakilisha majimbo ya Tiverton na Honiton huko Devon tangu mwaka 2010, alisema imekuwa wakati wa wazimu.

Alisema mara ya kwanza ilikuwa bahati mbaya baada ya kuangalia tovuti ya trekta kisha akakutana na video za ngono, lakini mara ya pili katika Baraza la Commons, ilikuwa ya makusudi na anajutia.

Alisimamishwa kazi na Chama cha Conservative siku ya Ijumaa kutokana na madai hayo.

Wabunge wenzake wawili wa kike walidai kuwa walimwona akiangalia maudhui ya watu wazima kwenye simu yake akiwa ameketi karibu nao.

Katika mahojiano maalum na BBC, Parish alisema: Hali ilikuwa ya kuchekesha, ni matrekta niliyokuwa nikitazama.

"Niliingia kwenye tovuti nyingine iliyokuwa na jina linalofanana sana na niliitazama kwa muda, jambo ambalo sikupaswa kufanya."

"Lakini uhalifu wangu ni uhalifu mkubwa ni kwamba katika tukio lingine nilienda mara ya pili."

Alikiri kwamba mara ya pili ilikuwa ya makusudi na kwamba ilitokea katika Baraza la Commons alipokuwa ameketi kusubiri kupiga kura.

Alisema alichokifanya ni makosa kabisa na kuongeza: Itanibidi kuishi na hili maisha yangu yote. Nilifanya kosa kubwa sana na niko hapa kuuambia ulimwengu." **BBC**

HABARI MICHEZO

# MPOLE HAWAZII TU KIATU CHA DHAHABU LIGI TANZANIA BARA

**Na Dennis Fussi**

MSHAMBULIAJI wa Geita Gold, George Mpole, amesema hata asipokuwa mfungaji bora msimu huu, lakini anaridhishwa na mafanikio aliyoipa timu hiyo kutokana na mabao yake.

Mshambuliaji huyo anayeshika nafasi ya pili akiwa na mabao 11, amesema kazi ambayo ameifanya mpaka sasa inaonyesha kwamba hajababatisha bali ni kutokana na bidii na ushirikiano mzuri kutoka kwa wenzake.

"Nafurahi kuona nipo kwenye kiwango bora msimu huu na hilo linathibitishwa na mabao yangu ambayo nimeyafunga, timu nyingi zikiwamo kubwa za Azam na Simba," alisema Mpole.

**Alisema kutokana na mbio za ufungaji bora zilivyokuwa ngumu, ataridhika hata ikitokea akashindwa kuibuka mshindi kwa sababu tayari ametimiza ipasavyo majukumu yake.**

Mpole alisema kwa nafasi waliyopo hivi sasa na mechi zilizobaki, anaamini Geita Gold itamaliza msimu huu kwenye nafasi tano za juu na hiyo itakuwa ni mafanikio makubwa kwake.

Mshambuliaji wa Yanga Fiston Mayele ndiye kinara wa mbio za kufunga hadi sasa akiwa na mabao 12.

Geita Gold ipo nafasi ya sita ikiwa na pointi 28 sawa na Mbeya City iliyopo nafasi ya tano ikiizidi kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa, huku Namungo yenye alama 29 katika nafasi ya tatu ikifungana pointi hizo na Azam FC iliyopo nafasi ya tano na mchezo mmoja mkononi.




Washindi wa 'Betika Mtoko wa Kibingwa' wakifurahia moja ya matukio kwenye mchezo wa watani wa jadi, Simba na Yanga uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Washindi Betika waichambua dabi*

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kushuhudia timu za Simba na Yanga zikitoshana nguvu kwa suluhu kwenye mchezo wa dabi juzi, washindi wa 'Betika Mtoko wa Kibingwa' wamechambua mechi hiyo ya watani wa jadi.

Washindi 24 kwenye promosheni ya Mtoko wa Kibingwa inayoendeshwa na kampuni ya michezo ya kubashiri walikuwa miongoni mwa maelfu ya mashabiki walioshuhudia dabi hiyo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi.

Washindi hao waliowasili Dar es Salaam kwa ndege wakitokea mikoa mbalimbali nchini na kugharamiwa huduma zote na Kampuni ya Betika, wameondoka jana na wengine wanne kutoka Tabora na Mtwara wakitarajiwa kuondoka leo.

Wakizungumza kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), baadhi ya washindi hao ambao ni mashabiki wa Simba na Yanga wamechambua dabi hiyo huku wale wa Yanga wakiwatania wa Simba kuwa wamewakosakosa.

Peter Martin wa Singida, ambaye ni mnazi wa Simba alisema hiyo ni mara ya kwanza kwake kuishuhudia dabi hiyo laivu na kuishukuru Betika kwa kuwapa fursa washindi wake.

Alisema licha ya timu yake kutoka sare, amevutiwa zaidi na kiwango cha beki wa Simba, Henoc Inonga.

"Inonga ni beki makini, anacheza mpira bila madhara, binafsi, ni beki ambaye ananivutia kwenye kikosi cha Simba," alitoa kauli sawa na iliyotolewa na Dismas Elias wa Dodoma ambaye ni mnazi wa Simba.

Amon Mdao wa Dodoma ambaye ni Yanga lialia, yeye alisema kama si Onyango (Joash) na Inonga, Simba ilikuwa inapasuka katika mechi hiyo ya juzi.

"Wamefanya kazi kubwa kuzuia mashambulizi, lakini bahati yao tumewakosakosa, japo sare kwetu si mbaya, bado tunaongoza ligi na hakuna kufungwa hadi ubingwa," alijiaminisha.

Meneja Uhusiano wa Betika, Nelson Saimon, alisema Promosheni ya Mtoko wa Kibingwa imefanyika kwa mafanikio makubwa.

"Washindi wote 24, wameitizama dabi kwa hadhi ya VIP kuanzia walipowasili Dar es Salaam kwa wale waliotoka mikoa," alisema.

Alisema baada ya Betika Mtoko wa Kibingwa kufikia tamati, mambo makubwa zaidi yanakuja ikiwamo kwenye EPL na Kombe la Dunia, hivyo mashabiki wa Betika wakae mkao wa kucheza na kushinda.

## TFF sasa yakaribisha maombi tiketi Kombe la Dunia

**Na Adam Fungamwango**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limesema baada ya Sikukuu ya Id El Fitri, litaanza kupokea maombi ya mashabiki watakaokata tiketi kwa ajili ya kwenda nchini Qatar kushuhudia fainali za Kombe la Dunia, zinazotarajiwa kuchezwa baadaye mwaka huu.

Taarifa ya TFF iliyotolewa jana na kusainiwa na Ofisa Habari na Mawasiliano wake, Cliford Ndimbo, imeeleza kuwa shirikisho hilo litaanza kupokea maombi hayo, baada ya Sikukuu ya Idd El Fitri, hivyo kuwataka mashabiki wanaotaka kwenda kutazama michuano hiyo kuchangamkia maombi hayo.

Aidha, limewataka mashabiki watakaoomba tiketi hizo kidijitali waambatanishe taarifa zao kadhaa, ikiwamo jina la kwanza, na la ukoo, tarehe ya kuzaliwa, utaifa, nakala ya hati ya kusafiria, pamoja na nchi anayotoka kwenye hiyo tiketi.

Taarifa hiyo imetaja mwisho wa kupokea maombi hayo ni Mei 12, mwaka huu, huku waombaji wote wakitakiwa kutuma maombi yao kupitia barua pepe jacqueline.kamwamu@tff.or.tz.

Hata hivyo, imetahadharisha kuwa mchakato unaofanyika sasa ni maombi tu, na siyo uthibitisho wa kupata tiketi. Wale watakaothibitishiwa kupata tiketi hizo wataelekezwa jinsi ya kufanya malipo.

Michuano hiyo ambayo itafanyika kwa mara ya kwanza barani Asia, itaanza kutimua vumbi nchini Qatar kuanzia Novemba 21 na kumalizika Desemba 18, mwaka huu ikizishirikisha jumla ya timu 32, ikiyashirikisha mabara sita ambayo yataumana kulisaka kombe hilo ambalo kwa sasa linashikiliwa na Ufaransa ambayo ililitwaa mwaka 2018 nchini Russia.



## ZISIKUPITE

### GUARDIOLA KUONGEZEWA

KLABU ya Manchester City inaamini Pep Guardiola atasaini mkataba mpya mwishoni mwa msimu, huku mazungumzo yakifanyika kuhusu kumuongezea Mhispania huyo muda wa kuendelea kukaa hapo City hadi mwaka 2025. ***(Sunday Mirror)***

### WARD-PROWSE AGOMBEWA

MANCHESTER City na Manchester United zinataka kumsajili kiungo wa England, James Ward-Prowse, 27, kutoka Southampton, wakati Arsenal, Newcastle United na Tottenham zikifuatilia kwa karibu maendeleo ya nyota huyo. ***(Daily Star on Sunday)***

### DEMBELE AIKATALIA PSG

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Ousmane Dembele, 24, ametangaziwa ofa nono kutoka klabu ya Paris St-Germain kuliko ile ya klabu yake ya Barcelona, lakini mwenyewe chaguo lake ni kubakia Nou Camp ambapo mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Sport)***

### TORRES ATAKIWA EPL

MANCHESTER City na Manchester United zinapigana vikumbo kuwania saini ya mlinzi wa kati wa Hispania, Pau Torres, 25, kutoka Villarreal. ***(Todofichajes)***

### TEN HAG AMTAKA MALACIA

ERIK ten Hag ambaye ataondoka Ajax kwenda kuwa kocha mkuu wa Manchester United mwishoni mwa msimu huu, anataka kumsajili mlinzi wa kushoto wa Feyenoord na Uholanzi, Tyrell Malacia, 22. ***(Sunday Mirror)***

### DE JONG TEGEMEO BARCA

KIUNGO wa Uholanzi, Frenkie de Jong amekuwa akihusishwa na klabu ya Manchester United, lakini Kocha wa Barcelona, Xavi, 24, ni tegemeo la sasa na la baadaye la klabu hiyo ya Hispania. ***(Manchester Evening News)***

### DORTMUND NA HALAAND

MTENDAJI Mkuu wa Klabu ya Borussia Dortmund, Hans-Joachim Watzke amesema klabu hiyo iliishinda Manchester United kwenye mbio za usajili wa Erling Haaland, 21, Desemba 2019 kwa sababu walijiandaa kumuwekea nyota huyo wa kimataifa wa Norway kipengele katika mkataba wake kinachozungumzia kuruhusiwa kuondoka ikiwa kiasi fulani cha fedha kitatolewa. ***(Goal)***

### JAMES KUFUNGWA CHELSEA

CHELSEA watamuongezea mkataba bora zaidi mlinzi wa kulia wa England, Reece James, 22, ambaye amekuwa akihusishwa na Real Madrid. ***(90 Min)***

### REGUILON KUREJESHWA MADRID

REAL Madrid itawalazimu kutumia hadi dola milioni 33.5 kumrejesha mlinzi wa kushoto wa Hispania, Sergio Reguilon, 25, kutoka Tottenham Hotspur. ***(Todofichajes)***

### NEVES KUPELEKWA SOKONI

KLABU ya Wolves ipo tayari kumuuza kiungo wake, Ruben Neves, 25, huku klabu hiyo ya West Midlands ikitarajia kuongeza nguvu katika kikosi chake kwa kusajili washambuliaji na viungo wapya. ***(Sunday Times )***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ANCELOTTI NA NJAA YA MATAJI BAADA LALIGA

### Najivunia,nataka kuendelea kushinda makombe nikiwa na Real Madrid, tuonane...

**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti alielezea nia yake ya kushinda mataji zaidi akiwa na Real Madrid baada ya 'Los Blancos' hao kunyakua taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga, kwa ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Espanyol, Jumamosi.

Mabao mawili ya kipindi cha kwanza ya Rodrygo yaliwaweka vijana wa Ancelotti mbele kabla ya Marco Asensio na Karim Benzema kila mmoja kufunga moja pale kwenye Uwanja wa Santiago Bernabeu.

Madrid walitwaa taji lao la 35 la Ligi Kuu Hispania huku wakiwa wamebakisha michezo minne, hivyo kuwafanya wabebe taji hilo mapema zaidi tangu msimu wa 1989-99.

**Ancelotti amekuwa kocha wa kwanza kushinda kila ligi kati ligi tano kubwa za Ulaya na Muitaliano huyo ana njaa ya mafanikio zaidi, huku akiwa kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambao kwenye mchezo wa kwanza walipoteza kwa mabao 4-3 dhidi ya Manchester City, Jumatano iliyopita.**

"Hisia nyingi, tumekutana na changamoto," alisema Ancelotti mara baada ya mchezo huo.

"Msimu umekuwa wa kuvutia. Uthabiti mwingi. Lazima niwashukuru wachezaji kwa kazi yao na mtazamo wao.

"Leo (juzi) tunatakiwa kusherehekea, sio kuzungumza, nataka kusherehekea. Inanijaza fahari kushinda katika ligi kuu tano, naweza kusema napenda ninachofanya, maana yake nimefanya vizuri.

"Najivunia. Nataka kuendelea kushinda mataji nikiwa na Real Madrid. Tuonane Jumatano. Ninawaambia mashabiki Jumatano tunahitaji hali hii [dhidi ya Manchester City kwenye mechi ya nusu fainali ya pili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya]."

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
MANCHESTER UTD
VERSUS
BRENTFORD
1 | 1.79
X | 3.62
2 | 4.10

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# GUARDIOLA: UBINGWA UPO MIKONONI MWETU CITY



**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amesisitiza kwamba, hatima ya timu yake ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England iko mikononi mwao.

Man City imeipita Liverpool kwa pointi moja baada ya timu zote kushinda mechi zao za Jumamosi dhidi ya Leeds United na Newcastle United.

Kikosi cha Guardiola kilishinda mabao 4-0 kwenye Uwanja wa Elland Road na kufikisha pointi 83 zikiwa zimesalia mechi nne.

Ingawa kocha huyo mwenye umri wa miaka 51, anaheshimu uzito wa hali hiyo na anaamini kwamba upinzani ni mkubwa dhidi ya Liverpool.

"Kila kitu kipo mikononi mwetu," alisema Guardiola baada ya mechi hiyo.

"Wolves, Newcastle, West Ham na Aston Villa, lazima tuwashinde wote na tutakuwa mabingwa, lakini tukiacha pointi, Liverpool watakuwa mabingwa.

"Tunajua kile tunachohitaji kufanya - kushinda michezo yetu.

"Bado ni bahati na heshima kujaribu kushinda mataji, tunatakiwa kushinda kila mechi."



# Haaland amlilia Raiola

**DORTMUD,** Ujerumani

ERLING Haaland ametuma salamu za rambirambi kwa kifo cha wakala wake, Mino Raiola, ambaye alifariki dunia Jumamosi akiwa na umri wa miaka 54.

Familia ya Raiola ilitangaza kuwa aliaga dunia Jumamosi, siku mbili baada ya kubainika kuwa Muitaliano huyo alikuwa katika hali mbaya katika hospitali ya San Raffaele mjini Milan.

Mmoja wa mawakala wanaotambulika duniani, Raiola aliwakilisha mastaa kama Haaland, Zlatan Ibrahimovic, Paul Pogba na wengine wengi.

Haaland aliweka picha ya pamoja yeye na Raiola na kuandika kwenye ukura wake wa Instagram: "Wewe bi bora."

Naye mshambuliaji wa Juventus, Moise Kean pia alitoa rambirambi zake.

Aliandika kwenye Instagram: "Bado siamini, ulinitoa mitaani na umenifanya nijifunze kanuni nyingi sana za maisha, kusema kweli sio kwaheri kwetu popote ulipo utaendelea kuwa kwangu siku zote. R.I.P BIG Boss."

Familia ya Raiola ilisema katika taarifa: "Kwa huzuni kubwa tunashiriki kifo cha wakala anayejali na wa kush gaza wa mpira wa mig kuwahi kutokea.

"Mino alipamb hadi mwisho kwa n vu zile zile alizoziw kwenye meza za n zungumzo kuwate wachezaji wetu. Ka kawaida, Mino alituf ya tujivunie kuwa nay

"Mino aligusa mai ya watu wengi kup kazi yake na kuand ukurasa mpya kat historia ya soka ya k sa. Uwapo wake utaku bukwa milele.

"Dhamira ya M ya kufanya soka ku mahali pazuri zaidi k wachezaji itaendelea shauku sawa.

CHEZA USHINDE KASINO
JISAJILI
CHEZA
SHINDA

# BENKI NBC YAING'ARISHA 'DERBY' YA KARIAKOO

Na Mwandishi Wetu

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC), ambayo ni mdhamini Mkuu wa Ligi Kuu ya Soka la Tanzania Bara (NBC Premier League), jana iliipamba mechi ya watani wa jadi katika soka la Tanzania, Simba na Yanga kwa kuandaa matukio kadhaa kwa ajili ya wapenzi wa mchezo huo pamoja na wateja wa benki hiyo ikiwamo kukabidhi tuzo na zawadi kwa mchezaji bora na kocha bora wa mwezi Machi, mwaka huu katika ligi hiyo.

Shughuli zote hizo ziliongozwa na maofisa waandamizi wa benki hiyo wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Theobald Sabi, ambaye alipata wasaa wa kukabidhi tuzo na zawadi ya fedha kiasi cha Sh. milioni moja, kwa mchezaji wa klabu ya Simba Clatous Chama, alietangazwa mchezaji bora wa ligi hiyo kwa mwezi Machi sambamba na Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Pablo Franco ambaye pia alitangazwa kocha kwa mwezi huo na hivyo kuzawadiwa tuzo pamoja na fedha kiasi hicho kutoka kwa mdhamini mkuu.

**Tukio hilo lilishuhudiwa na maelfu ya mashabiki waliojitokeza kutazama mechi hiyo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, lilitanguliwa na matukio mengine mengi ikiwamo mapokezi ya wateja wa benki hiyo kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini waliobahatika kuibuka washindi katika Droo ya Jaza Kibubu Na NBC.**

Washindi hao walipata fursa ya kushuhudia mechi hiyo wakiwa wamelipiwa gharama zote ikiwamo za usafiri, malazi sambamba na kupatiwa tiketi za VIP kwa ajili ya kushuhudia mtanange huo uliomalizika kwa sare ya bila kufungana.

Pamoja na washindi hao, benki hiyo pia iliandaa mwaliko rasmi kwa ajili ya wateja wake mashuhuri wakiwamo viongozi waandamizi kutoka mashirika na taasisi mbalimbali na wadau wengine wa benki hiyo waliopata wasaa kupata chakula cha mchana pamoja na viongozi wa NBC kisha kwa pamoja walielekea Uwanja wa Benjamin Mkapa kushudia mechi hiyo wakiwa katika msafara maalum.

Aidha, mashabiki waliojitokeza kutazama mechi hiyo walipata fursa ya kupata huduma mbalimbali za kifedha kutoka benki ya NBC kupitia maofisa wake mbalimbali waliokuwa wakitoa huduma hizo kwenye viunga vya uwanja huo, hatua iliyotoa fursa kwa mamia ya mashabiki hao kujiunga na huduma za benki hiyo ikiwamo kufungua akaunti mbalimbali pamoja na kufanya miamala ya kifedha wakiwa maeneo hayo.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, ambaye ni mdhamini Mkuu wa Ligi Kuu ya Soka ya Tanzania Bara (NBC Premier League), Theobald Sabi (kushoto) akikabidhi tuzo kwa kocha wa Klabu ya Simba, Pablo Franco, aliyetangazwa kocha bora wa ligi hiyo kwa mwezi Machi, wakati wa mechi kati ya timu hiyo na Yanga iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi na kumalizika kwa sare tasa. **MPIGAPICHA WETU**

# Mbeya City yataja tatu za malengo

Na Saada Akida

KOCHA Mkuu wa Mbeya City, Mathias Lule, ametaja mechi tatu za ushindi ili kujihakikishia kufikia malengo yake ya kumaliza msimu huu wakiwa katika nafasi nne za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mechi hizo tatu za Mbeya City ni dhidi ya Mtibwa Sugar utakaopigwa katika dimba la Manungu, Turiani mkoani Morogoro na michezo miwili watakayocheza katika Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya dhidi ya Azam FC na Polisi Tanzania. Akizungumza na gazeti hili jana, Lule alisema anatambua kuna vita kubwa ya kuwania nafasi ya nne katika msimamo wa ligi hiyo, ila ameanza na mechi hizo tatu kutafuta pointi tisa ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kufikia malengo yao.

Alisema wakati huu ligi ikielekea ukingoni timu zinapambana kuhakikisha zinafikia malengo yao, hivyo nao watahakikisha wanapambania pointi tatu katika kila mechi kwa lengo la kufikia kile wanachokihitaji msimu huu.

"Ili kufikia malengo yetu lazima tucheze kwa nidhamu ya hali ya juu, mipango yetu ni kuanza na mechi tatu zilizopo mbele yetu kuhakikisha tunashinda hizo ili kujiweka salama katika kitu tunachokitafuta msimu huu," alisema kocha huyo.

Alisema ushindani unakuwa mkubwa kwa sababu ya timu zinazoshika nafasi kuanzia ya tatu kushuka chini kutofautiana pointi chache, na zidi ikiwa moja.

"Tuna pointi 28 na tuko nafasi ya tano aliyekuwa nafasi ya tatu na ya nne wametupia pointi moja, ambao ni Namungo na Azam FC, nina matarajio ya kufanya vizuri michezo hiyo kufikia malengo yetu," alisema Lule.

Katika msimamo wa Ligi Kuu, Yanga inaongoza kwa pointi 55 ikifuatiwa na Simba yenye alama 42.

SPORTPESA APP
PAKUA APP YETU,
BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI
"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 02/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 4382 | Salford City vs Mansfield | 2.39 | 3.26 | 2.82 |
| 16:00 | 2557 | Waterford Utd vs Athlone Town | 1.21 | 5.83 | 9.52 |
| 17:00 | 1088 | Dartford vs Braintree | 1.75 | 3.75 | 4.30 |
| 17:00 | 1210 | Blyth Spartans vs Curzon | 2.48 | 3.31 | 2.53 |
| 17:00 | 1475 | Southport vs Telford | 2.26 | 3.17 | 2.92 |
| 17:00 | 1496 | Kettering Town vs Alfreton | 1.78 | 3.55 | 3.89 |
| 17:00 | 1590 | Altrincham vs Barnet | 1.89 | 3.80 | 3.40 |
| 17:00 | 2131 | Port Vale vs Newport | 1.90 | 3.32 | 3.96 |
| 17:00 | 2244 | Eastleigh vs Halifax | 3.49 | 3.39 | 1.99 |
| 17:00 | 2399 | Solihull Moors vs Bromley | 1.71 | 3.80 | 4.24 |
| 17:00 | 2498 | Boreham Wood vs Wrexham | 3.79 | 3.39 | 1.90 |
| 17:00 | 2725 | Darlington vs Farsley Celtic | 1.48 | 3.98 | 5.83 |
| 17:00 | 2962 | Welling vs Maidstone | 5.46 | 3.99 | 1.50 |
| 17:00 | 3023 | Notts County vs Dover | 1.17 | 6.50 | 12.81 |
| 17:00 | 3117 | Maidenhead U vs Aldershot | 2.04 | 3.41 | 3.31 |
| 17:00 | 3185 | Wexford Youths vs Bray Wanderers | 2.08 | 3.30 | 3.16 |
| 17:00 | 3792 | Oxford City vs St.Albans | 1.71 | 3.64 | 4.17 |
| 17:00 | 3906 | York City vs AFC Fylde | 2.85 | 3.35 | 2.37 |
| 17:00 | 4008 | Chester vs Bradford PA | 1.63 | 3.80 | 4.49 |
| 17:00 | 4083 | Woking vs Kings Lynn | 1.64 | 3.94 | 4.54 |
| 17:00 | 4119 | Yeovil vs Wealdstone | 1.83 | 3.50 | 3.94 |
| 17:00 | 4337 | Chorley vs Gateshead | 3.89 | 3.60 | 1.77 |
| 17:00 | 4438 | Southend vs Weymouth | 1.58 | 3.88 | 5.11 |
| 17:00 | 4462 | Boston Utd vs Gloucester City | 1.71 | 3.56 | 4.29 |
| 17:00 | 4726 | Billericay Town vs Ebbsfleet | 5.00 | 3.90 | 1.62 |
| 17:30 | 4612 | CS Mioveni vs Botosani | 2.25 | 3.03 | 3.27 |
| 19:00 | 1920 | Arsenal Tula vs Nizhny Novgorod | 2.35 | 3.03 | 3.08 |
| 19:00 | 5562 | Cork City vs Treaty United | 1.43 | 4.09 | 6.42 |
| 19:15 | 5295 | Fulham vs Luton Town | 1.50 | 4.15 | 5.74 |
| 19:30 | 1499 | Leganes vs Huesca | 2.53 | 2.97 | 2.87 |
| 19:30 | 1714 | Asteras Tripolis vs Lamia | 1.88 | 3.07 | 4.56 |
| 19:45 | 2269 | Chambly vs Laval | 3.96 | 3.21 | 1.92 |
| 20:00 | 1076 | IFK Goteborg vs Kalmar | 2.21 | 3.07 | 3.11 |
| 20:00 | 4043 | Norrkoping vs IFK Varnamo | 1.61 | 3.69 | 4.76 |
| 20:00 | 5006 | Silkeborg vs Aalborg | 1.95 | 3.54 | 3.59 |
| 20:10 | 5583 | Hammarby vs Malmo | 2.33 | 3.42 | 2.64 |
| 20:30 | 5089 | Hapoel Tel Aviv vs Maccabi Haifa | 5.62 | 3.83 | 1.51 |
| 20:30 | 5248 | Chesterfield vs Stockport | 3.95 | 3.16 | 1.94 |
| 20:30 | 5955 | Steaua Bucuresti vs Argesul Pitesti | 1.32 | 4.66 | 9.32 |
| 21:00 | 2752 | KA Akureyri vs Keflavik IF | 1.58 | 3.97 | 4.65 |
| 21:30 | 1559 | Bayer Leverkusen vs Eintracht Frankfurt | 1.40 | 4.96 | 6.15 |
| 21:30 | 3851 | Monchengladbach vs RB Leipzig | 4.04 | 3.90 | 1.74 |
| 21:45 | 1107 | Rodez Aveyron vs Toulouse | 4.96 | 3.42 | 1.71 |
| 21:45 | 1185 | Atalanta vs Salernitana | 1.25 | 5.74 | 9.69 |
| 22:00 | 1219 | Valladolid vs Real Sociedad B | 1.35 | 4.83 | 7.50 |
| 22:00 | 2154 | Manchester Utd vs Brentford | 1.79 | 3.62 | 4.10 |
| 22:00 | 5206 | Getafe vs Betis | 2.70 | 3.05 | 2.70 |
| 22:15 | 4515 | Fram Reykjavik vs IA Akranes | 2.68 | 3.41 | 2.30 |
| 22:15 | 4903 | Pacos Ferreira vs Tondela | 2.22 | 3.23 | 3.18 |
| 22:15 | 5556 | Vikingur Reykjavik vs Stjarnan | 1.55 | 4.07 | 4.75 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Mei 2, 2022


Nipashe




'Ubingwa upo mikononi mwetu City'

UKURASA 22

HAPO MWISHO...



Beki wa kati wa Simba, Henoc Inonga 'Varane', akiucheza mpira kuokoa hatari dhidi ya mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi na kumalizika kwa sare tasa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Pablo, Kaze nao waichambua dabi

**Na Saada Akida**

MAKOCHA waliobeba dhamana ya kuziongoza timu zao kwenye mechi ya 'dabi' ya watani wa jadi, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco na Mwalimu Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, kila mmoja ametoa tathimini yake baada ya timu hizo kutoka suluhu katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi.

Akizungumza baada ya mechi hiyo kumalizika, Pablo alisema hawajafurahishwa na sare ya bila kufungana waliyopata dhidi ya Yanga kwa kuwa lengo lilikuwa kupata pointi zote tatu ambazo zingewafanya kuwasogelea zaidi wapinzani wao hao, lakini matokeo hayo yameipa nafasi Yanga kuwa karibu na ubingwa, ingawa hawajakata tamaa hadi mwisho wa msimu.

Alisema mchezo ulikuwa mzuri uliotawaliwa na mbinu ingawa washambuliaji na nyota wake walipaswa kutumia vizuri nafasi walizotengeneza.

"Sijafurahishwa na matokeo ya sare, tuliingia kwa nia ya kutafuta ushindi kwa kuwa tunahitaji kupunguza tofauti iliyopo na bado tunahitaji kutetea ubingwa wetu," alisema Pablo.

Kwa upande wa Kaze, alisema kipindi cha kwanza hakikuwa kizuri kwao licha ya kutengeneza nafasi na kushindwa kuzitumia kwa sababu ya wachezaji wao kutofanya maamuzi sahihi huku dakika 20 za mwisho walifanya makosa na kuwafanya Simba wamiliki zaidi mpira.

"Tulifanikiwa kuziba njia zote za Simba hasa kutoruhusu beki zao kupanda na kupeleka mashambulizi, pia hata sisi hatukuwa vizuri katika kumalizia licha ya kufika ndani ya 18," alisema Kaze.

# Inonga: Sikutaka Mayele 'ateteme'

**Na Saada Akida**

### ●●● Asema lengo lilikuwa kumnyima nafasi ya kutimiza ahadi yake, Kaze amtetea...

BAADA ya kuonyesha kabumbu safi kwa kumkaba na kumnyima raha uwanjani mshambuliaji wa Yanga na kinara wa mabao Ligi Kuu Bara, Fiston Mayele, beki kisiki wa Simba, Henoc Inonga 'Varane' amesema hakuwa tayari kumuona Mcongoman mwenzake huyo, akitetema mbele yake katika pambano hilo la watani wa jadi 'Kariakoo Derby', lililopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi.

**Katika mchezo huo, uliooshuhudiwa miamba hiyo ikishindwa kufungana kwa mara ya pili msimu huu baada ya kutoka suluhu kama ilivyokuwa mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo inayoelekea ukingoni kwa sasa.**

Wiki moja kabla ya mchezo huo, Mayele aliahidi kuwa ana deni kwa mashabiki wake la kutimiza kuifunga Namungo FC na Simba, jambo ambalo alianza kulitimiza kwa kufunga dhidi ya timu hiyo ya Ruangwa mkoani Lindi na kusema sasa amebakiza kuitungua Simba, hivyo angeitungua juzi na kushangilia kwa staili yake ya kutetema.

Akizungumza na Nipashe baada ya mechi hiyo, Inonga alisema alilazimika kuhakikisha anakuwa makini na Mayele ili kutompa nafasi mshambuliaji huyo wa Yanga kutikisa nyavu zao halafu 'akatetema' mbele yake.

Inonga alisema amefanikiwa kumzuia na hakuweza kutetea na kwamba licha ya mchezo huo kuwa mgumu kwa kila upande, lakini malengo yake ya kutompa nafasi mshambuliaji huyo kutimiza ahadi yake yalifanikiwa kwa asilimia 100.

"Tumepambana, malengo yalikuwa pointi tatu, lakini tumepata moja ila nimefanikiwa kumzuia mtu asiteteme (No kutetema), licha ya kutoka nchi moja na kuonyesha ni mechi ya upande wetu hakuweza kutetema," alisema Inonga.

Lakini wakati Inonga akiyasema hayo, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, alimtetea Mayele kwa kutofunga katika mchezo huo, akieleza ni jambo la kawaida licha ya kutoa ahadi kwa sababu malengo yao yalikuwa kutafuta pointi na hilo wamefanikiwa.

"Hii mechi ni kati ya Simba dhidi ya Yanga na si Mayele dhidi ya Inonga, hajafunga lakini tumepata pointi moja na kutufanya tuendelee kujiamini katika malengo yetu," alisema Kaze.

Mayele ndiye kinara wa mabao hadi sasa kwenye Ligi Kuu msimu huu, akiwa amecheka na nyavu mara 12 akifuatiwa na George Mpole wa Geita Gold FC mwenye mabao 11.

Kwa matokeo ya mechi hiyo, yanaifanya Yanga kufikisha alama 55 kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo wakati huu ikibakiza mechi tisa kabla ya kufunga msimu huu, hata hivyo inafutiwa na Simba yenye pointi 42, lakini ikicheza mechi moja pungufu.

Simba itashuka tena dimbani kesho katika Uwanja wa Majaliwa mkoani Lindi kuwavaa wenyeji wao, Namungo FC waliopo nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo wakiwa na pointi zao 29 zilizotokana na mechi 21.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >